**Aliyebaka** mtoto agonga mwamba Mahakama Rufani

UKURASA 5



**Mwalimu** Mkuu kizimbani tuhuma za kughushi vyeti

UKURASA 5







UKURASA 11

Ijumaa Julai 16, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580643

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



# Vilio tozo za miamala simu

**Wachumi** waipa angalizo serikali, wahadharisha... *UK. 2*



Dk. Godbertha Kinyondo

## Mahakama kusikiliza ushahidi kesi ya Sabaya

UKURASA 2





Mradi mkubwa wa NHC wa Morocco Square, ulioko Manispaa ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Samia aingilia mradi wa NHC uliokwama miaka 7

UKURASA 4

**MICHEZO** HATIMA UCHAGUZI MKUU TFF LEO UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Mahakama kusikiliza ushahidi kesi ya Sabaya

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MASHAHIDI wa kesi namba 66 ya jinai ya mwaka 2021, leo wanatarajiwa kutoa ushahidi katika mashtaka mawili ya unyang'anyi kwa kutumia silaha, yanayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya na wenzake watano.

Julai 2, mwaka huu, Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha iliuagiza Upande wa Jamhuri kuhakikisha unawaandikia barua ya wito mashahidi kufika mahakamani kutoa ushahidi wa mashtaka mawili hayo.

Hakimu wa Mahakama hiyo, Salome Mshasha, alitoa agizo hilo baada ya kushindikana kusikilizwa kwa shauri hilo, Upande wa Jamhuri uliposhindwa kuwafikisha mahakamani mashahidi.

Wakili wa Serikali, Tarsila Gervas, alidai mahakamani huko siku hiyo kuwa shauri hilo lilipangwa kwa ajili ya kusikilizwa, lakini shahidi wa Upande wa Jamhuri alipata udhuru na kushindwa kufika mahakamani, hivyo kuomba mahakama kupanga tarehe nyingine ya kusikilizwa kwa shauri hilo.

Hata hivyo, Mawakili wa Upande wa Utetezi; Dankan Oola, Mosses Mahuna, Silvestar Kahunduga, Fredoline Gwemelo na Geston Justine, waliomba kuelezwa na Upande wa Jamhuri idadi ya mashahidi katika shauri hilo.

Leo, Sabaya na wenzake watano wanatarajiwa kupandishwa kizimbani kwa mara ya nne wakikabiliwa na mashtaka matano ya uhujumu uchumi, rushwa, kuongoza genge la uhalifu, utakatishaji wa fedha na unyang'anyi wa kutumia silaha. Mbali na Ole Sabaya, washtakiwa wengine ni msaidizi wake wa karibu, Silvester Stanslaus, Enock Togolani, John Odemba, Daniel Gabriel, na Waston Mwakomange.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na Rais wa Benki ya Afrika, Othman Benjelloun (kulia), kwenye hoteli ya Sofitel jijini Rabat, nchini Morocco, juzi. Habari Uk. 8. **PICHA: OWM**

# Vilio tozo miamala ya simu

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI tozo mpya za miamala ya simu zikianza rasmi jana, kilio kimesikika kutoka kwa wananchi wakilalamikia gharama kubwa katika miamala hiyo, huku wataalamu wa uchumi wakiishauri serikali kufanya tafakuri ya kina.

Kuanzia jana, kilio dhidi ya tozo mpya za miamala kupitia kampuni za simu vilisikika kupitia mitandao ya kijamii na kuzua mijadala kadhaa miongoni mwa watumiaji, wakipendekeza mbinu kadhaa za kukwepa kufanya miamala.

Mtaalamu wa Uchumi na Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Dk. Godbertha Kinyondo, akizungumza na Nipashe jana kuhusu suala hilo, alisema serikali inapaswa kukaa mezani na mamlaka zake ambazo ni Wizara ya Fedha na Mamlaka ya Mapato (TRA) kupitia upya tozo hizo.

"Ninachoona huu utaratibu mpya wa makato umekuja haraka, sijui kama serikali ilikaa chini na kufanya uchunguzi wa kina kwa sababu inaweza kuwaathiri watu hasa wafanyabiashara wadogo," alitahadharisha.

Dk. Godbertha alisema utaratibu wa benki kwa simu uliletwa kwa ajili ya watu wote kusaidia waingie katika sekta ya fedha kwa njia ya simu na kupitia mfumo huo wapate huduma kwa urahisi.

Alisema njia hiyo iliwafanya Watanzania wengi kuingia katika mfumo wa kifedha na ina faida kwao, serikali na uchumi kwa ujumla kwa kuwa imetengeneza mnyororo wa fedha.

Alisema watu waliweka fedha, kukopa, kufanya huduma za malipo na kusaidia kukuza uchumi wa Watanzania hasa wakazi wa vijijini waliokuwa wanapata huduma mbalimbali kwa njia hiyo.

Alisema tozo mpya zitaathiri serikali kwa sababu inaongeza kodi zake ambazo zinawaathiri wananchi wengi.

Alitahadharisha kuwa kutokana na ongezeko hilo la tozo za miamala, huenda serikali isikusanye tena kodi ya kutosha kupitia eneo hilo kwa sababu wananchi watatafuta njia mbadala za kutuma na kupokea fedha.

"Watu wana akili na watafuta njia mbadala za kutumiana fedha ili kukwepa makato hayo, lakini mwisho wa siku wataathiri mzunguko wa fedha za uchumi kwa ujumla uliokuwa unategemewa kwa njia ya simu," alisema Dk. Godbertha.

Alifafanua kuwa umuhimu wa fedha kwa njia ya simu umeoanishwa na kilimo, afya na elimu imeunganishwa na sekta nyingine zote na hivyo tozo mpya zitaathiri pia sekta hizo.

"Makato yakiwa rafiki, yataenda vizuri katika kukuza sekta hizo, lakini kama yalivyopanda, yataathiri sekta hizo zote," alifafanua.

Alisema njia ambazo zitatumiwa na watu ni watu wenyewe kusafirisha fedha na kwenda benki, hivyo tozo mpya zitaongeza foleni barabarani na mwisho wa siku Watanzania watarudi nyuma kiuchumi.

**KILIO CHA WANANCHI**

Mkazi wa Ukonga jijini Dar es Salaam, Alfred John, aliiambia Nipashe kwamba jana alifanya muamala kutoka mtandao wa simu ya mkononi na kukatwa kiasi ambacho ni mara mbili ya gharama ya awali.

Jumanne Mrisho alisema kwa wakulima ni hasara kubwa kwa sababu mara nyingi wanatuma fedha za pembejeo, lakini fedha za mazao wanatumiwa kwa njia ya simu, hivyo tozo mpya zitasababisha hasara kwao.

Mfanyabiashara mdogo, Sharon Emmanuel, alidai makato hayo ni makubwa kulinganisha na mapato ya kila siku ya Mtanzania.

**NJIA MBADALA**

Kutokana na kupanda kwa tozo hizo, baadhi ya wananchi waliozungumza na Nipashe jana, walisema njia ya kuepukana na miamala hiyo kwa sasa kutumia benki ambazo makato yake yako chini kulinganishwa na ya simu.

Baadhi ya wafanyabiashara wa magari ya kubeba abiria wanaopata wateja kwa njia ya mtandao, walisema makato hayo yatawagharibu kwa sababu wanapokea wateja ambao wakati mwingine hawana fedha taslimu.

Mwinyimkuu Hassan, dereva mwingine wa magari hayo, alisema kuwa kwa muda mrefu amekuwa akituma 'hesabu' za bosi kwa njia ya simu, lakini sasa inabidi aanze kutumia benki.

Mary Kishama alisema kutuma mzigo mkoani usiyo mzito ni kuanzia Sh. 5,000 kwa kampuni zinazosafirisha na ndiyo njia rahisi na salama anayoona ya kusafirisha fedha ili kuepuka usumbufu huo.

Alisema pia anaweza kusafiri kupeleka fedha eneo moja kwenda lingine katika mkoa wake kwa kutumia gharama ndogo isiyozidi 1,000 ili kukwepa makato hayo.

Baadhi ya wajasiriamali wadogo ikiwamo kinamama wanaojihusisha na vyama vya kuweka akiba na kukopeshana, waliiambia Nipashe kwamba kutokana na tozo za miamala katika kampuni za simu za mkononi kuongezeka, watabadili utaratibu wa kutuma na urejesha mikopo, sasa watahamia kwenye benki.

"Tuna umoja wetu mtaani, shughuli zetu tulio wengi ni biashara ndogo

●**Imeandaliwa na Mary Geofrey na Christina Mwakangale**


Palladium
MAKE IT POSSIBLE

HDIF

UKaid

## TAARIFA KWA UMMA:
## MRADI WA HDIF KUFIKIA TAMATI

Kampuni ya Palladium pamoja na washirika wake imekuwa ikiendesha Mfuko wa Ubunifu wa Maendeleo ya Binadamu (HDIF) unaofadhiliwa na Serikali ya Uingereza kupitia UKAID tangu Septemba 2013. Palladium imekuwa ikifanya kazi kwa ukaribu na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH).

HDIF ilianzishwa kwa lengo la kuchangia ubunifu katika utoaji wa huduma muhimu katika sekta ya Elimu, Afya na Maji na Usafi wa Mazingira (WASH) nchini Tanzania. Mfuko ulikuwa pia na lengo la kuchangia uendelezaji wa mfumo wa ubunifu kwa ujumla. Kwa zaidi ya miaka 7 iliyopita, HDIF ilijikita katika kutoa msaada wa kifedha na kiufundi kwa miradi ya ubunifu, kuchochea ubunifu wa Tanzania, na kuchangia uboreshaji wa mazingira wezeshi na rafiki ili ubunifu uweze kushamiri. Haya yalifanywa kwa njia ya mafunzo, majukwaa ya majadiliano, mikutano na mazungumzo na wadau muhimu. HDIF ilifanikiwa kufadhili miradi ya moja kwa moja 48 kwenye sekta husika. Mfuko pia ulifadhili 'startups' 27 kupitia mashindano ya ubunifu (innovation challenges). HDIF iliandaa na kufadhili semina, warsha na majukwaa mengi ya wadau ili kukuza ubunifu nchini, 'Wiki ya Ubunifu Tanzania' ikiwa ni jukwaa mojawapo lililojipatia umaarufu wa aina yake. Pia kwa kupitia COSTECH, HDIF ilifadhili bunifu 15 pamoja na kumbi za bunifu 15 (innovation hubs) ili kuzijengea uwezo zaidi. Kupitia kazi hizi na nyingine nyingi, ni dhahiri kwamba HDIF ilichangia ipasavyo katika ukuaji wa mfumo wa ubunifu nchini Tanzania.

Baada ya karibu miaka 8 ya utekelezaji, mradi wa HDIF utafungwa rasmi ifikapo 31 Julai 2021, ukiacha nafasi kwa jitihada nyingine kama Programu ya FUNGUO inayoratibiwa na UNDP kuendeleza pale HDIF ilipoachia.

Kwa mtu yeyote mwenye madai au mwenye kuhitaji maelezo zaidi kuhusu HDIF au Palladium Group Tanzania Ltd, tafadhali wasiliana na Mkurugenzi wa Fedha na Utawala wa HDIF Bwana Revocatus Vedasto kwa barua pepe **revocatus.vedasto@thepalladiumgroup.com**

116361202

NA UTAWALA

TANGAZO

# TAARIFA KWA UMMA

**Kufuatia marekebesho yaliyofanywa na serikali kupita sheria ya fedha ya mwaka 2021 na kwenye kifungu namba 46A (2) cha sheria ya Mfumo wa Malipo wa Taifa (National Payment Systems), Waziri wa Fedha kwa kushirikiana na Waziri wa Mawasiliano wamepewa mamlaka ya kutengeneza kanuni zitakazosimamia namna ya ukusanyaji wa tozo za serikali kwenye miamala ya kutuma na kutoa fedha kwa njia ya simu. Kanuni zimetolewa na Waziri wa Fedha kwa kupitia Notisi ya Serikali namba 496A iliyochapishwa tarehe 30 Juni 2021. Kufuatia marekebisho haya ya sheria, kampuni ya Tigo Pesa itaanza kukusanya tozo hizo kwa niaba ya serikali kuanzia tarehe 15 Julai 2021.**

***Lifuatalo ni jedwali linalonyesha aina ya tozo mbalimbali zitakazo tozwa kwa watumiaji wa simu kulingana na kiwango cha miamala itakayofanyika.***

tigo pesa

## Ni Zaidi ya Pesa

## Ada za wateja. Piga *150*01#

| Kiwango (Tsh) | | Kutuma pesa kwenda Tigo Pesa | | | Kutuma pesa kwenda mitandao washirika | | | Kutoa pesa kwa Wakala/ATM | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kuanzia | Mwisho | Ada ya Tigo Pesa | Tozo ya Serikali | Jumla ya Makato | Ada ya Tigo Pesa | Tozo ya Serikali | Jumla ya Makato | Ada ya Tigo Pesa | Tozo ya Serikali | Jumla ya Makato |
| 100 | 999 | 15 | - | 15 | 15 | - | 15 | - | - | - |
| 1,000 | 1,999 | 30 | 10 | 40 | 50 | 10 | 60 | 300 | 10 | 310 |
| 2,000 | 2,999 | 30 | 16 | 46 | 50 | 16 | 66 | 400 | 16 | 416 |
| 3,000 | 3,999 | 50 | 27 | 77 | 100 | 27 | 127 | 600 | 27 | 627 |
| 4,000 | 4,999 | 60 | 56 | 116 | 100 | 56 | 156 | 650 | 56 | 706 |
| 5,000 | 6,999 | 130 | 100 | 230 | 200 | 100 | 300 | 950 | 100 | 1,050 |
| 7,000 | 9,999 | 150 | 125 | 275 | 200 | 125 | 325 | 1,000 | 125 | 1,125 |
| 10,000 | 14,999 | 360 | 320 | 680 | 550 | 320 | 870 | 1,450 | 320 | 1,770 |
| 15,000 | 19,999 | 360 | 610 | 970 | 550 | 610 | 1,160 | 1,450 | 610 | 2,060 |
| 20,000 | 29,999 | 380 | 960 | 1,340 | 600 | 960 | 1,560 | 1,850 | 960 | 2,810 |
| 30,000 | 39,999 | 400 | 1,100 | 1,500 | 680 | 1,100 | 1,780 | 1,850 | 1,100 | 2,950 |
| 40,000 | 49,999 | 410 | 1,500 | 1,910 | 750 | 1,500 | 2,250 | 2,350 | 1,500 | 3,850 |
| 50,000 | 99,999 | 720 | 2,050 | 2,770 | 1,250 | 2,050 | 3,300 | 2,700 | 2,050 | 4,750 |
| 100,000 | 199,999 | 1,000 | 2,530 | 3,530 | 1,600 | 2,530 | 4,130 | 3,650 | 2,530 | 6,180 |
| 200,000 | 299,999 | 1,200 | 2,940 | 4,140 | 1,900 | 2,940 | 4,840 | 5,300 | 2,940 | 8,240 |
| 300,000 | 399,999 | 1,500 | 3,500 | 5,000 | 2,300 | 3,500 | 5,800 | 6,500 | 3,500 | 10,000 |
| 400,000 | 499,999 | 1,500 | 4,100 | 5,600 | 2,500 | 4,100 | 6,600 | 7,000 | 4,100 | 11,100 |
| 500,000 | 599,999 | 2,200 | 5,200 | 7,400 | 3,200 | 5,200 | 8,400 | 7,500 | 5,200 | 12,700 |
| 600,000 | 699,999 | 3,300 | 6,400 | 9,700 | 4,300 | 6,400 | 10,700 | 8,000 | 6,400 | 14,400 |
| 700,000 | 799,999 | 3,300 | 7,100 | 10,400 | 4,300 | 7,100 | 11,400 | 8,000 | 7,100 | 15,100 |
| 800,000 | 899,999 | 3,500 | 7,520 | 11,020 | 4,300 | 7,520 | 11,820 | 8,000 | 7,520 | 15,520 |
| 900,000 | 1,000,000 | 3,500 | 8,900 | 12,400 | 6,000 | 8,900 | 14,900 | 8,000 | 8,900 | 16,900 |
| 1,000,001 | 3,000,000 | 5,000 | 9,400 | 14,400 | 6,000 | 9,400 | 15,400 | 8,000 | 9,400 | 17,400 |
| 3,000,001 | 10,000,000 | 5,000 | 10,000 | 15,000 | 6,000 | 10,000 | 16,000 | 10,000 | 10,000 | 20,000 |

| Tukio | Kuanzia | Mwisho | Ada |
|---|---|---|---|
| Kuweka pesa | 1,000 | 5,000,000 | BURE |
| Kutuma pesa kwa mteja ambaye hana akaunti ya Tigo Pesa au akaunti ya mitandao washirika | 1,000 | 1,000,000 | Ada ya kutuma + Ada ya kutoa |
| Kutoa Pesa kwa mteja ambaye amesajiliwa ila hana akaunti ya Tigo Pesa au akaunti ya mitandao washirika | 1,000 | 1,000,000 | BURE |
| Kutuma pesa kwenda nchi za nje | 100 | 5,000,000 | Kulingana na kiwango |
| Malipo kwa Tigo Pesa | 500 | 5,000,000 | Kulingana na kiwango |

| Tukio | Ada |
|---|---|
| Kubadilisha namba ya siri | BURE |
| Kuangalia salio/ Taarifa ndogo | 50 |
| Kurudisha muamala uliokosea (Jihudumie) | 50 |
| **Kupata taarifa ya mwezi** | **Ada** |
| Taarifa ya Mwezi jana/Mwezi huu | BURE |
| Taarifa ya Miezi 3 | 1,000 |
| Taarifa ya Mwaka 1 | 2,000 |

Kwa vigezo na masharti ya huduma tembelea tovuti: https://www.tigo.co.tz/tigo-pesa-standard-terms-and-conditions. **Ada zote zimejumuisha kodi zote zinazohusika.**
Kwa Ada za huduma nyingine tembelea tovuti; **https://www.tigo.co.tz/tigo-pesa-tariffs**

**Furahia Malipo kwa Tigo Pesa:** LIPA KWA SIMU

**KUMBUKA:**

1. Unaweza kuweka au kupokea hadi TSh 5,000,000 kwa siku na unaweza kutoa au kutuma hadi TSh 5,000,000 kwa siku, pia unaweza kuhifadhi hadi TSh 10,000,000 kwa wakati mmoja kwenye akaunti yako ya Tigo Pesa, kama usajili wako umekamilika.
2. Onesha kitambulisho chako kabla ya kuweka au kutoa pesa kwa Wakala.
3. Hakikisha taarifa zako za usajili ni sahihi kwa kupiga *106# kisha 2 au piga huduma kwa wateja kwa maelezo zaidi.
4. Hesabu pesa zako na hakikisha salio lako la Tigo Pesa linaendana na muamala uliofanya kabla ya kuondoka kwa Wakala.
5. Kila mara unapotuma pesa, kumbuka kuhakiki namba ya mpokeaji kuepuka kukosea na usumbufu.
6. Hakikisha unahifadhi namba yako ya siri (PIN), simu yako na laini yako kwa usalama. Usimpe (PIN, Simu, laini yako) wala kumtajia mtu yoyote namba yako ya siri, iwe Wakala wa Tigo Pesa, mfanyakazi wa Tigo au mhudumu wa Tigo Huduma kwa wateja. Pia kumbuka kubadili namba yako ya siri mara kwa mara.
7. Tigo itakupigia kwa 0713800800 au 0713123103 Tu.
8. Kutoa taarifa yoyote dhidi ya udanganyifu Piga simu namba 100 au tuma ujumbe kwa barua pepe kwenda customercare@tigo.co.tz
9. Unaweza kupokea pesa kutoka nchi zaidi ya 200 duniani, na unaweza kutuma pesa kwenda nchi zote za Afrika Mashariki.
10. Kupata vigezo na masharti ya kutumia Tigo Pesa, tembelea duka la Tigo lililopo karibu nawe au www.tigo.co.tz

Unaweza kurudisha **muamala uliokosea**, **token ya luku**, **ku-unbar akaunti yako ya Tigo Pesa** na **kuriseti PIN**

Piga ***150*01#** chagua **6 (Jihudumie)** kisha chagua huduma unayotaka

tigo pesa

**App yenye urahisi wa kushangaza!**




**Fanya malipo ya Serikali**

Pakua kwenye

Google Play | App Store

tigo pesa

Kuwasaliana na huduma kwa wateja,
Piga **100** bure au tembelea duka lolote la Tigo!
Ada hizi ni kuanzia July 2021

tigo

www.tigo.co.tz

116359802

MAKALA MAALUM

# Samia aingilia mradi NHC wa bil. 137/- uliogota miaka 7

## •Unatajwa hauna mpinzani EAC
## •Ni kati ya minne iliyokwama

**Na Romana Mallya**

RIPOTI ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2019/20, mbali na mambo mengine, inanyooshea kidole miradi iliyogharimu mabilioni ya shilingi, lakini sasa haitumiki.

Vilevile, uchambuzi wa ripoti hiyo iliyotua bungeni Aprili mwaka huu, uliofanywa na Taasisi ya WAJIBU, hauko nyuma katika kuimulika miradi iliyotafuna mabilioni ya shilingi, lakini haitumiki au kubadilishwa matumizi.

Miradi ya ujenzi inayotekelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) maeneo mbalimbali nchini, ni sehemu ya kilio cha wadau hao.

Ufuatiliaji wa Nipashe kuhusu suala hilo, umebaini kuwa baada ya kusimama kwa miaka minne, mradi mkubwa wa NHC wa Morocco Square ulioko Kinondoni mkoani Dar es Salaam, unatarajiwa kumaliziwa miezi miwili ijayo ili nyumba hizo zikabidhiwe rasmi kwa wateja.

Mradi huo ulioanza kutekelezwa Juni 2014 ukitarajiwa kukamilika mwanzoni mwa mwaka 2017, ulisimama mwaka 2017 baada ya ujenzi wake kuanza kusuasua mwaka 2015 kutokana na wanunuzi wa mauzo ya kabla ya jengo kukamilika kupungua.

Mradi huo ambao unatajwa kuwa mkubwa zaidi wa nyumba Afrika Mashariki na Kati, ujenzi wake unatarajiwa kugharimu Sh. bilioni 137.5 na ni miongoni mwa miradi minne mikubwa ya NHC iliyosimama kwa kipindi kirefu.

Mingine iliyosimama ni pamoja na wa Kawe unaoitwa Seven Eleven (711) ukiwa na thamani ya Sh. bilioni 105, ambao kwa sasa unasubiri kukamilika kwa mradi wa Morocco ndipo nao uendelezwe.

Mradi mwingine wa shirika hilo uliomo kwenye orodha hiyo, ni wa Golden Premier Residence (GPR) ulioko Barabara ya Mwai Kibaki wenye thamani ya Sh. bilioni 71.

Kijiografia, mradi huo uko mbele ya ule wa Kawe 711 na mradi wa nne ni ulioko kwenye Kiwanja Na. 300 (Ada Estate) wenye thamani ya Sh. bilioni 24.2.

Katika mahojiano maalum na Nipashe jijini Dar es Salaam, Meneja Habari na Uhusiano wa NHC, Muungano Saguya, anabainisha kuwa ili kuliepusha shirika kupata hasara iliyotahadharishwa na wadau, akiwamo CAG na Taasisi ya WAJIBU, wamekuwa wakijenga nyumba kwa mtindo wa kuziuza wakati zikiendelea kujengwa.

"Tunafanya pre-sell (mauzo ya kabla) kabla jengo halijakamilika, hili limesaidia shirika kupunguza utegemezi wa mikopo kutoka katika taasisi za fedha. Hali hii pia imefanya miradi yetu iweze kujiendesha yenyewe.



Sehemu ya majengo ya mradi wa mji mpya wa Kawe, Manispaa ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam. **PICHA: MAKTABA**

"Ni ukweli usiofichika kipindi fulani miradi kama Morocco Square na ule wa Kawe 711 ilitetereka kwa mtindo wa pre-sell, watu wanaojitokeza kununua nyumba kabla haijakamilika, walipungua kwa sababu ulikuwa utamaduni mpya kwa Watanzania, huo ndio ukweli.

"Baada ya kupungua na kwa sababu tulitarajia kupata fedha za wateja na kuzitumia kuzungusha kwenye ujenzi, miradi ile kama Morocco Square na Kawe 711 (Dar es Salaam) ikasimama," anafafanua.

Anabainisha kuwa mwaka 2015, utamaduni wa watu kununua kabla ulianza kulegalega na hadi kufikia mwaka 2017 ujenzi ulisimama kwa sababu makandarasi walishindwa kutekeleza majukumu yao kwa kuwa walitarajia walipwe fedha.

"Ili kuwalipa fedha ilikuwa ni lazima tuombe kibali cha mwenye mali ambaye ni serikali kwa maana ya Hazina, ili tupate kibali cha kukopa fedha kwa ajili ya kumalizia ujenzi.

"Kama unavyojua serikali lazima nayo ijiridhishe kuwa 'hawa (NHC) tukiwaruhusu kukopa watakuwa na uwezo wa kuilipa mikopo', nalo ni mchakato mrefu kidogo mpaka ijiridhishe.

"Ninaweza kusema Serikali ya Awamu ya Sita ya Rais Samia Suluhu Hassan imeshalikubalia shirika sasa kuweza kukopa.

"Hii ni miradi mikubwa ambayo kwa sasa serikali imeruhusu NHC kukopa Sh. bilioni 174 ili kuikamilisha. Serikali ya Awamu ya Sita pia imetupatia Sh. bilioni 20 ili tuanze kuukamilisha mradi wa Morocco Square," anafafanua.

Anasema kwa sasa shughuli za ujenzi zinaendelea Morocco na mwishoni mwa Septemba wataanza kuwapatia wateja wao maeneo yao.

"Huu ni mradi mkubwa na wa kipekee ambao umelala katika sakafu moja (msingi mmoja), una mita za mrada 110,000, ndani yake zimo sehemu za ofisi, biashara, hoteli, maduka makubwa, wakati wa malipo ya kabla wateja walinunua makazi katika mradi huu karibu asilimia 60.

"Lakini kama unavyojua, watu walisuasua kuendelea kulipa hapo awali, kwa sasa wanavyoona unaendelea vizuri, wameanza kufanya malipo," anasifu.

**WAREJESHEWA FEDHA**

Saguya pia anabainisha kuwa wapo wateja waliofikia hatua ya kuomba kurejeshewa fedha zao na NHC ililazimika kufanya hivyo, lakini anasita kuanika idadi yao.

"Unakuta mtu labda alitaka kupata nyumba akae, sasa anaona muda unakwenda, akachukua fedha zake lakini kwa nia njema ya Serikali ya Awamu ya Sita, imeidhinisha Sh. bilioni 20 ambazo zinasaidia ujenzi wa Morocco Square kuendelea na tumeruhusiwa kukopa.

"Tukimaliza hapa Morocco, tutahamia Kawe 711 kwenye mwaka huu wa fedha na kumalizia miradi mingine iliyobaki," anasema.

Anabainisha kuwa miradi yao imegawanyika katika sehemu tatu, akifafanua kuwa wanajenga nyumba za makazi kwa watu wa kipato cha chini kiasi, kati na cha juu na kwa mradi wa Morocco Square unahusisha kipato cha juu ukiwa na nyumba 100.

Anabainisha kuwa mradi huo una vyumba 81 kwa ajili ya hoteli na wanaviuza na vingine vinapangishwa.

Saguya anasema mradi huo wa Morocco Square wakati unasimama mwaka 2017, ulikuwa umekamilika kwa asilimia 90 na hadi Julai 13 mwaka huu, ulikuwa umefikia asilimia 96.

**UFAFANUZI KWA JK**

Aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa NHC, Nehemiah Mchechu, wakati anamkaribisha Rais wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, kuweka jiwe la msingi kwenye mradi huo Oktoba 7, 2015, alisema unatekelezwa na mkandarasi ambaye ni kampuni ya Kitanzania ya Estim Construction Ltd ya Dar es Salaam.

Alisema mradi huo ulitarajiwa kugharimu Sh. bilioni 150 ambazo ni mkopo kutoka Benki ya CRDB.

Alisema kati ya mita za mraba 110,000 za mradi huo, mita 47,793 ni kwa ajili ya ofisi, mita 24,929 za makazi na mita 28,827 ni kwa ajili ya makazi wakati kumbi za biashara, maduka makubwa, sehemu za kuchezea watoto na maduka ya vyakula na hoteli zikiwa na ukubwa wa mita za mraba 8,456.

Alisema mradi huo una uwezo wa kubeba watu 6,000 na kutoa ajira zipatazo 24,750 kwa majengo manne tofauti, ikiwamo ghorofa 22 kwa ajili ya nyumba 100 za makazi zenye vyumba vitatu na vinne, ghorofa 20 na 17 kwa ajili ya ofisi na maduka makubwa na ghorofa 13 kwa ajili ya hoteli yenye vyumba vya kulala 81.

Mchechu alifafanua kuwa mradi huo pia una eneo maalum la kutua chopa na eneo kubwa kwa ajili ya maegesho ya magari.

**MIRADI YA NHC**

Katika mahojiano hayo maalum na Nipashe, Saguya anasema shirika linamiliki zaidi ya majengo 18,000 kwenye maeneo mbalimbali ambayo ni kwa ajili ya kupangisha (makazi) na ya shughuli za biashara.

"Nyumba hizi tulikuwa tunapangisha pamoja na taasisi za serikali lakini sehemu kubwa tunapangisha Watanzania kwa matumizi mbalimbali, nyumba zinazomilikiwa na NHC ni asilimia moja tu au chini ya asilimia moja ya mahitaji ya nyumba kwa Watanzania," anasema.

Saguya anasema nyumba wanazomiliki kwa maana ya kupangisha na biashara hazizidi asilimia moja ya idadi ya nyumba zilizopo nchini.

**KUHAMIA DODOMA**

Anasema kuwa baada ya uamuzi wa serikali kuhamia Dodoma, shirika halijaathirika kwa kiwango kikubwa kwa kuwa mahitaji ya nyumba hata kabla ya uamuzi huo yalikuwa makubwa.

"Watu walikuwa wanaendelea kuleta maombi yao lakini wanakosa, wanaambiwa wasubiri, ziwe za kupangisha au shughuli za biashara.

"Baada ya serikali kwenda Dodoma, yale majengo ambayo tulipangisha, mfano lile la Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Holland House ilikuwa Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo iliyochukua Idara ya Habari (MAELEZO), yote yalipata wapangaji wapya.

"Hatukutikisika sana, ingawa mwanzo unaweza kupata wapangaji wengine wa haraka haraka huwa ni shida, lakini baada ya muda tuliwapata na walijaa, hatukupata hasara yoyote," anasisitiza.

Saguya anasema nyumba walizozijenga maeneo ya Kibada na Mwongozo wilayani Kigamboni, zote zilipata wateja ndani ya saa 24 baada ya kukamilika.

# Aliyebaka mtoto agonga mwamba Mahakama Rufani

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Rufani Tanzania imebariki Vedastus Emmanuel kuendelea kutumikia kifungo cha maisha jela kwa kubaka mtoto wa miaka minane wilayani Tarime.

Jopo la majaji watatu, Gerald Ndika, Particia Fikirini na Dk. Paul Kihwelo, lilitoa uamuzi huo baada ya Emmanuel kukata rufani kupinga uamuzi wa Mahakama ya Wilaya ya Tarime kumtia hatiani na kumpa adhabu ya kifungo cha maisha jela.

Alikata rufani Mahakama Kuu mbele ya Jaji Mohamme Gwae wa Kanda ya Mwanza, lakini ikatupwa akakimbilia Mahakama ya Rufani ambako pia imeonekana haina msingi na kutupwa.

Mrufani alishtakiwa akidaiwa kuwa Desemba 23, 2015 saa 1:00 usiku mtaa wa Rhebu wilayani Tarime, alimbaka mtoto wa miaka minane.

Katika ushahidi wake, mtoto anadai alikutana na mrufani katika uwanja wa mpira wa Serengeti, akamwita jina kisha akamshika mkono na kumpeleka nyumbani kwake ambako ni jirani na anakoishi.

Alidai kuwa mrufani alimwingiza katika chumba ambacho kilikuwa na kitanda, meza na kitandani palitandikwa shuka jeupe.

Inadaiwa alimlaza kitandani, akamvua nguo na kumwingilia huku akimsababishia maumivu makali na alipomaliza alimpeleka kuoga, akaenda kumnunulia biskuti na pipi kisha akamtoa nje.

Ushahidi unaeleza kwamba mtoto alianza kutafutwa na kwamba Anna Chenge akiwa anamtafuta, alimwona akitokea nyumbani kwa mrufani, hivyo kutoa taarifa kwa mama yake.

Mashahidi hao walipomhoji mtoto alieleza jinsi alivyobakwa na walitoa taarifa polisi. Mtoto alichunguzwa na daktari, alibainika kwamba hana bikira.

Binti alieleza alizaliwa Mei 7, 2007 na wakati akifanyiwa tendo hilo alikuwa na miaka minane.

Mrufani alipinga adhabu aliyopewa akidai kwamba Mahakama ilikosea kuzingatia ushahidi wa mtoto wa kuunga unga, shahidi wa pili na wa tatu hawakupewa taarifa ya tukio na kwamba katika maelezo ya awali haikuelezwa kwamba shahidi wa tatu atakuwa miongoni mwa mashahidi wa Jamhuri. Sababu ya mwisho anadai utetezi wake haukuzingatiwa na mahakama katika kutoa uamuzi.

Baada ya kupitia hoja za rufani na hoja za Jamhuri, jopo lilibaini kwamba ushahidi ulithibitika, ushahidi wa shahidi wa kwanza ambaye ni mtoto ulikuwa wa kweli na alieleza tukio lilivyokuwa na alithibitisha umri wake.

Jopo hilo linasema mrufani katika utetezi wake hakugusia siku ya tukio Desemba 23, 2015.

"Rufani haina msingi wowote. Inakataliwa na kutupwa," lilisema jopo hilo katika hukumu.

Baada ya rufani kutupwa, mrufani ataendelea kutumikia adhabu ya kifungo cha maisha aliyopewa na Mahakama ya Wilaya ya Tarime na Mahakama Kuu kubariki na hatimaye Mahakama ya Rufani.




Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi (kushoto), akiagana na mgeni wake Balozi wa Ethiopia nchini Tanzania, Yonas Yosef Sanbe, baada ya kujitambulisha na mazungumzo yao, Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Mwalimu Mkuu kortini kwa tuhuma za kughushi vyeti

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Dodoma imemfikisha mahakamani Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Karume wilayani Kongwa kwa tuhuma za kughushi vyeti vya darasa la saba na kuviuza kwa Sh. 50,000 kila kimoja.

Inadaiwa kuwa mwalimu huo alighushi vyeti hivyo kwa ajili ya kuwauzia wanaojiunga na Mafunzo ya kujitolea ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema jana jijini hapa kuwa mtuhumiwa huyo pamoja na aliyejifanya mhitimu wa shule huyo, juzi walifikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Kongwa.

Alisema hadi mwalimu huyo anakamatwa alikutwa ametoa vyeti viwili kwa Mbaraka Juma na Elia Fred wote wakazi wa Kata ya Kibaigwa mkoani Dodoma.

"Tumemfikisha pia aliyejifanya mwanafunzi mhitimu wa shule hiyo, Mbaraka Juma, kwa tuhuma za kutoa nyaraka za uongo ya kuwa amehitimu darasa la saba katika shule hiyo wakati si kweli ili atimize vigezo vya kujiunga na mafunzo ya JKT," alisema.

Alisema TAKUKURU kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka, wamefikisha mahakamani hapo watuhumiwa hao na baada ya kusomewa shtaka linalowakabili walipata dhamana na wapo nje kusubiri kesi yao kutajwa. Kibwengo aliwataka wananchi kutoa taasisi za viashiria au vitendo vya rushwa kwenye maeneo mbalimbali wanayofanyia shughuli zao.

Alisema mapambano ya rushwa ni ya jamii kwa ujumla na si TAKUKURU peke yake ndiyo maana wamekuwa wakitoa elimu kwa wananchi kupambana na vitendo hivyo.

"Wananchi wasisite kutoa taarifa pale wanapoona zinaviashiria vya rushwa ili tuzifanyie uchunguzi kabla ya kuchukua hatua stahiki za kiutendaji kazi."

"Tunaomba wananchi mwendelee kutoa ushirikiano wa utoaji taarifa za kiuhalifu tunahitaji kuona rushwa inatokomezwa kwa sababu ni adui wa haki," alisema Kibwengo.

# SADC yapiga jeki ujenzi barabara

**Na Gwamaka Alipipi**

JUMUIYA ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), imeipatia Tanzania Dola za Marekani milioni sita (Sh. bilioni 13.850), kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa reli kutoka Mtwara hadi Mbamba bay.

Ujenzi wa reli hiyo utafungua fursa za maendeleo katika korido ya maendeleo Mtwara, kukuza mtandao wa biashara kati ya Tanzania na nchi za Malawi, Msumbiji, Zambia kwa kupunguza gharama za usafirishaji na kuboresha uchumi kwa bidhaa za ndani na nje.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Mipango wa Zanzibar, Jamal Kassim Ali, alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kabla ya kuanza kwa kikao cha mawaziri wa fedha na uwekezaji wa SADC.

Alieleza: "Baada ya kupokea fedha hizo kinachofuata kwa sasa ni kuanza kufanya upembuzi yakinifu, kisha tutapata makandarasi wa kujenga reli hiyo kutoka Mtwara-Songea-Mbamba bay".

Alifafanua kwamba kukamilika kwa reli hiyo kutasaidia kukua kwa uchumi kwa mikoa ya kusini, kwamba mizigo kutoka nchi jirani itasafirishwa kwa wepesi.

Waziri Ali alisema mawaziri hao wa fedha pia wamekubaliana kuanzishwa kwa mfuko wa maendeleo wa SADC ambao utakuwa unafadhili miradi ya maendeleo ya nchi wanachama wote pindi inapohitaji kutekelezwa.

Kadhalika, alieleza kuwa wanachama wa SADC wameafikiana kuituma Afrika Kusini katika nchi wanachama wa G-20 kuelezea changamoto ambazo wanachama wa SADC wanakabiliana nazo ikiwamo ongezeko la riba kutoka katika mikopo.

"Afrika Kusini ni miongoni mwa mwanachama wa nchi zenye uchumi mkubwa duniani (G-20), hivyo tumekubaliana kumtuma akatusemee kwamba nchi za SADC zinakabiliwa na changamoto ya riba kubwa katika urejeshaji wa mikopo. Hivi sasa dunia inakabiliwa na ugonjwa wa corona na nchi nyingi zimeathirika kiuchumi, hivyo mpango wa kuahirisha kulipa madeni uendane na zuio la kuongezeka kwa riba za mikopo," alisema Waziri Ali.

Serikali ipo katika mkakati wa upanuzi wa Bandari ya Tanga, Dar es Salaam na Mtwara, lengo ni kupanua biashara na kurahisisha usafirishaji wa bidhaa.

Mbali na hilo, ipo katika hatua za ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) yenye urefu wa kilometa 2,561 itakayounganisha mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma, Katavi pamoja na nchi jirani za Rwanda, Burundi, DRC, lengo kukuza uchumi na kuboresha maisha ya wananchi.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tozo hizi mzigo kwa wananchi

**JANA** kampuni za simu zilianza kutekeleza tozo mpya iliyopitishwa kwenye Bajeti ya mwaka 2021/22 ambayo ni kukata kati ya Sh. 10 hadi 200 kwa siku kwenye kila vocha ambayo mtumiaji ataweka, na kutoza kati ya Sh. 10 hadi 10,000 kwa kila muamala wa fedha, ambao mhusika atafanya.

Kodi hii ilipewa jina la kodi ya uzalendo na ilipitishwa na Bunge ikielezwa inakwenda kusaidia nchi kupata fedha zitakazoelekezwa kwenye miradi ya barabara vijijini, elimu, afya na maji lengo ni kuboresha huduma kwa wananchi hasa waishio vijijini.

Katika siku za mwanzo za utekelezaji imekuwa ni maumivu kwa wananchi hasa kodi ya miamala kwa kuwa hasa sasa mwananchi anakatwa tozo ya mtoa huduma, kodi ya serikali na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) katika kila muamala atakaoufanya.

Tozo ya kampuni inatofautiana kutoka kampuni moja hadi nyingine. Lakini kodi ya serikali nayo inatofautiana kulingana na viwango vya watumaji au wapokeaji, vivyo hivyo kwa kodi ya VAT.

Jana wananchi wengi walipata mshtuko pale walipofanya miamala kutokana na makato kuwa makubwa, lakini hofu inayoibuliwa kuwa kuna uwezakano mkubwa kutokea athari ukiwamo mfumuko wa bei hasa ikizingatiwa kwa sasa mafuta yamepanda bei lita moja ya petroli kufikia Sh. 2,405.

Mathalani, mtandao wa Tigo kwa sasa makato yanaanzia Sh. 310 kwa anayetoa kwa wakala/ATM kati ya Sh. 1,000 hadi 1,999 na kwa anayetoa kati ya Sh. milioni 3 hadi milioni 10 anakatwa Sh. 20,000, huku anayetuma kwenda mitandao mingine anakatwa Sh.15 kwa anayetuma Sh. 100 hadi 999 wakati anayetuma kati ya Sh. milioni 3 hadi milioni 10 anakatwa Sh. 15,000.

Aidha, kutuma fedha Tigo kwenda Tigo ni Sh. 15 kwa kiwango cha Sh. 100 hadi 1,999, huku anayetuma Sh. milioni 3 hadi milioni 10 atakatwa Sh. 15,000.

Mtandao mwingine gharama zake ni ukitoa Sh. 100,000 kwa wakala unakatwa Sh. 6,100 ikiwa imepanda kutoka Sh. 3,600 wakati kwa kiwango cha juu cha milioni 3 ilikuwa Sh. 10,000 na sasa ni 20,000.

Katika moja ya mtandao mtu alitoa Sh. 60,000 kwa wakala akakatwa Sh.4,750 ikiwa ni ada ya kampuni ya simu Sh. 2,700, kodi ya serikali Sh. 2,050.

Mjadala uliopo kwenye mitandao ya kijamii kuwa gharama ya kutuma na kutoa fedha husika ni kubwa kuliko nauli ya muhusika kuja kuchukua, na wengi wanasema ni bora kupanda basi kwenda kuchukua.

Kodi hii ina lengo jema la kuboresha huduma za kijamii, lakini kuna hofu huenda ikasababisha athari nyingine ya kupungua kwa ajira kwa maana sasa wengi hawatatumia huduma za simu kutuma au kupokea fedha, bali wataanza kutumia huduma za benki.

Kwa sasa anayenunua umeme kwa simu au kulipia huduma nyingine kama za maji basi anakatwa fedha mara mbili; kwa maana nyingine utalipia Luku na wakati huo huo utalipia kodi ya majengo, jambo ambalo ni mzigo mkubwa kwa mwananchi wa kawaida.

Pia kutokana na ongezeko hilo, kuna uwezekano mkubwa wa wananchi kuanza kuficha fedha ndani au kutembea nazo nyingi, huku wengi wataanza kutumia mawakala na benki zaidi kuliko mitandao ya simu, hivyo kudumaza biashara nyingine.

Kama suala hili halitachukuliwa kwa umakini, kuna uwezekano wa kutokea athari zaidi kwa wananchi na uchumi wa kwa ujumla. Ipo haja ya kuliangalia suala hili kwa jicho la pili kwa kuzingatia kuwa miamala ya simu inatumiwa na wengi wakiwamo wa vijijini wenye kipato kidogo.

Kadhalika, itaongeza foleni barabarani, kwa kuwa wengi wataamua kupeleka fedha wenyewe na wakati huo huo watu watapoteza muda mwingi barabarani badala ya kutumia kuzalisha. Athari nyingine inayoweza kutokea ni kupungua mzunguko wa fedha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Biashara Machinga ni sawa, lakini si katika mazingira haya



Na Sabato Kasika

**JUHUDI** mbalimbali zimekuwa zikifanyika kwa ajili ya kuwawekea wamachinga mpangilio mzuri wa kufanya biashara katika maeneo yasiyo rasmi, wakati maeneo yao yakiandaliwa, lakini utekelezaji wake umekuwa ukikwama.

Unakwama kutokana na baadhi yao kuhama na kwenda kando ya barabara, hali ambayo ni hatari kwa usalama wao kwa kuwa ajali za magari zikitokea zinaweza kuwakumba.

Hivyo kumekuwapo na wimbi la kuzagaa wamachinga maeneo mbalimbali mitaani na kuendesha biashara zao, wakiwamo hao wanaopanga kando ya barabara, hali ambayo ni hatari kwa usalama wao.

Hilo linatokana na ajali za magari zinapotokea, ni rahisi kwao kugongwa au biashara kuathiriwa, kwa kuwa mazingira kama hayo ya kupanga biashara maeneo hayo ni rahisi kufikiwa.

Kutokana na hali hiyo, sasa Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, linawataka kuacha kufanya biashara ndani ya barabara kwa ajili ya usalama wao na mali zao.

Binafsi ninaamini kwamba uamuzi huo ni mzuri na wenye lengo la kuokoa maisha ya wafanyabiashara hao, kwani mazingira wanayofanyia shughuli zao si salama na pia si vyema kusubiri majanga yatokee ndipo kitafute ufumbuzi.

Mratibu wa Polisi Makao Makuu Kikosi cha Usalama Barabarani, Mosi Ndozero, anasema, machinga wamekuwa wakihatarisha maisha yao kwa kufanya biashara barabarani.

Anachosema ni ukweli mtupu, kwani wapo wanaopanga biashara zao kandokando ya barabara kuanzia asubuhi hadi usiku na wengine waliopo sokoni, huwafuata wenzao wa barabarani wakati wa jioni.

Badala ya kufanyia biashara sokoni, barabara zinageuzwa kuwa masoko, hivyo bahati mbaya ikitokea ajali, ni rahisi watu wengi kukumbwa, hivyo suala la wamachinga kuondoka kwenye maeneo hayo nadhani lina umuhimu wake.

Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani kinasema kimekuwa kikitoa elimu kwa wamachinga kuhusu haki, wajibu na madhara ya kufanya biashara hizo kwenye mazingira hayo, kwa nini hali bado?

Rai hiyo kwa wafanyabiashara hao ya kutofanya biashara kandokando ya barabara, ingefaa kuchukuliwa kwa uzito wake na wahusika kwa lengo la usalama wao na wa wateja wake.

Mbali na kuhatarisha maisha yao kwa kupanga biashara kandokando ya barabara, wamachinga pia wamekuwa wakisababisha kero kwa 'kuvamia' njia za waenda kwa miguu na kupanga biashara zao.

Kwa kauli hiyo ya Kikosi cha Usalama Barabarani, ingekuwa ni vyema sasa kila mdau kushiriki ili kuhakikisha wamachinga wanafanya biashara zao katika mazingira rafiki kuliko ilivyo sasa.

Ingawa wamachinga wanatakiwa kufanya biashara kusumbuliwa katika maeneo walipo, baadhi yao wamekuwa wakitumia nafasi hiyo vibaya kwa kusogea hadi kandokando ya barabara na kupanga bidhaa zao.

Wakurugenzi wa halmashauri, wakuu wa wilaya na wa mikoa hawana kuchukulia kwa uzito kauli ya kikosi hicho kwa ajili ya usalama wa wafanyabiashara hao, kwani usalama ni muhimu zaidi.

Viongozi hao walishaelekezwa kuwatengea masoko kwa ajili ya wamachinga ili waondokane na mazingira hayo, lakini hilo ni kama halijatekezwa, hivyo wanapotakiwa kutoka barabarani, viongozi wajitokeze na kutenga masoko.

Jukumu la kutenga masoko kwa ajili ya wamachinga ni lao na hawawezi kulikwepa, hivyo ni vibaya kujitokeza na kulipatia ufumbuzi wa kudumu sakata la kuzagaa ovyo kwa wamachinga mitaani.

Ni hivi karibuni, Watanzania wameambiwa kuwa wamachinga wameingiza serikalini Sh. bilioni 46.71 zilizotokana na vitambulisho vya ujasirimali vilivyotolewa na serikali mwaka 2018.

Kwa mantiki hiyo, wana umuhimu katika maendeleo ya taifa, kwa kuwa ni miongoni mwa walipa kodi, hivyo suala la kuwatengea masoko rasmi na kuwahimiza kufuata sheria ni la muhimu.

Hadi Kikosi cha Usalama Barabarani kufikia kuwaambia wasifanyie biashara barabarani, ni wazi kwamba sasa inatosha ili wasije kukumbwa na ajali za magari kikosi hicho kikaonekana hakifanyi kazi.

# Aeleza bosi wake alivyotishiwa bastola

**Na Kulwa Mzee**

SHAHIDI katika kesi ya mfanyabiashara aliyemtishia mwenzake kwa bastola, Peter Mtwango(43), ameieleza mahakama alivyoshuhudia mshtakiwa akimtishia bosi wake. Shahidi alidai hayo juzi katika Mahakama ya Wilaya ya Ilala mbele ya Hakimu Mfawidhi, Martha Mpaze.

Katika kesi hiyo Mfanyabiashara wa Kariakoo, Adelard Lyakurwa, anashtakiwa kwa kumtishia kumuua kwa bastola mfanyabiashara maarufu, Valence Lekule.

Inadaiwa Julai 30, mwaka jana, maeneo ya Kariakoo, mitaa ya Mbaruku na Swahili, Wilaya ya Ilala, mshtakiwa akiwa na lengo la kuua, alimtishia Valence Lekule kumuua kwa kutumia bastola huku akijua kufanya hivyo ni kosa la kisheria.

Mtwango akiongozwa na Wakili wa Serikali Nancy Mshumbusi, alidai kuwa yeye ni mlinzi kutoka kampuni ya binafsi ya ulinzi iliyoingia mkataba wa kulinda nyumba ya Lekule.

Alidai kuwa Julai 30, 2020, aliingia lindo saa 2:00 usiku katika nyumba hiyo ya biashara iliyoko katika kiwanja namba 8, Kariakoo, mtaa wa Swahili na Mbaruku.

Alidai kuwa akiwa kazini hapo, Lekule alikwenda kuwatembelea walinzi wake na aliegesha gari barabarani hatua tatu kutoka kilipo kibaraza cha nyumba hiyo kisha akafungua dirisha la gari wakaanza kuzungumza Peter Kazee na Lekule.

Mtwango alidai kuwa wakati huo yeye alikuwa amebeba bunduki mgongoni mara akaona gari likija kwa kasi limewasha taa mpaka mwisho na kusimama huku likilizuia kwa mbele gari la Lekule.

Alidai kuwa alimwona mshtakiwa Lyakurwa akishuka kwenye gari hilo huku akiwa ameshika kitu mkononi cheusi na alipokiangalia vizuri kilikuwa bastola.

"Niliweza kuiona kuwa ni bastola kwa sababu katika eneo hilo kulikuwa na taa za barabarani, taa za nyumba ninayolinda na za majirani hivyo kulikuwa na mwanga wa kutosha.

"Alipofika katika gari ya Lekule, Lyakurwa alimshika mkono na kumwambia shuka chini leo nitakuonyesha mimi ni nani. Shuka chini nikuonyeshe mimi ni nani," alidai shahidi.

Alidai ghafla polisi waliokuwapo doria eneo hilo walitokea na kumhoji Lyakurwa kwa nini anafanya hayo na baada ya hapo waliondoka naye katika gari lao kwa nguvu na baadaye gari lake likafuatwa.

Baada ya kuondoka, alidai Lekule alipata nafasi ya kuondoka na hakujua kilichoendelea baada ya hapo.

Katika kesi hiyo, mshtakiwa huyo anatetewa na wakili wa kujitegemea Richard Mbuli.

Kesi hiyo iliahirishwa mpaka Julai 20, mwaka huu kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa kwa ushahidi wa mashahidi wengine.



Waziri wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba (katikati), akionyesha kadi namba moja aliyopewa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya Tanzania Commercial (TCB), Edmund Mndolwa (kushoto), wakati wa uzinduzi wa benki hiyo jijini Dar es Salaam juzi. Kulia ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki hiyo, Sabasaba Moshingi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Fursa za taasisi za fedha kukopa nyumba zaanikwa

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imetoa wito kwa Watanzania kutumia huduma ya taasisi za fedha za utoaji wa mikopo ya nyumba ya muda mrefu inayofikia mpaka miaka 25 ili kuongeza mapato ya ziada na kuchangia ukuaji wa uchumi.

Kamishna wa Idara ya Maendeleo ya Sekta Ndogo ya Fedha wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Charles Mwamwaja, aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati wa hafla ya kuorodheshwa kwa toleo la tatu la hatifungani ya Kampuni Mikopo ya Nyumba (TMRC) kwenye soko la Hisa (DSE).

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Mwamwaja alisema kwa sasa ni takriban miaka miwili tangu toleo la pili la hatifungani ya TMRC itolewe Julai Mosi, mwaka 2018 na sasa wapo katika uorodheshaji wa toleo la tatu la miaka mitano.

"Tumeshuhudia kuongezeka muda wa mikopo ya nyumba kutoka miaka mitano mpaka saba, na mingine kutoka miaka 15 mpaka 25, uwapo wa TMRC umewezesha benki kuanza kutoa mikopo ya nyumba na pia idadi ya benki zinazoshiriki utaratibu huu zimeongezeka kwa kiasi kikubwa," alisema.

Alisema faida ya mfumo huo ni kutoa nafasi ya kuwekeza kwenye nyumba kama sehemu ya mtaji ambazo zinamsaidia mmiliki kuwa na mapato ya ziada, kuchangia kodi za serikali kupitia mapato ya mwenye nyumba na kuinua uchumi.

Alisema TMRC imeanza kutafuta fedha za kukopesha taasisi za fedha kwa ajili ya mikopo ya nyumba kwenye soko la fedha ambapo shughuli hiyo inachangia kiasi kikubwa katika kukua kwa masoko ya mitaji.

Alisema TMRC imefanikiwa kutoa toleo lake la tatu la hatifungani ambalo linaonyesha makusanyo yamezidi matarajio kwa asilimia 27.

"Wakati toleo hili linaorodheshwa matarajio yalikuwa ni kukusanya Sh. bilioni 7 lakini wamekusanya Sh. bilioni 8.89. Washiriki wa toleo hili la tatu ni wawekezaji wa ndani na nje ambao wamekuwa na imani kinachofanywa Tanzania.

Alisema serikali ilianzisha mradi wa mikopo ya nyumba kwa kuchukua mkopo Benki ya Dunia (WB) wa Dola za Marekani milioni 100 na kuwezesha kuwapo kwa mfumo wa mikopo kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Nyumba.

Alisema kati ya fedha hizo TMRC ilikopeshwa Dola milioni 70 na hadi sasa imeshatoa hatifungani za jumla ya kiasi cha Sh. bilioni 30.59 katika mpango wake wa miaka mitano wa kutoa Sh. bilioni 120.

Mtendaji Mkuu wa TMRC, Oscar Mgaya, alisema toleo la tatu ni mwendelezo wa matoleo baada ya la kwanza la mwaka 2018 na la pili la mwaka 2019 ambayo yalipita malengo kwa asilimia mbili na asilimia nne kwa kila toleo.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa DSE, Moremi Marwa, alizitaka taasisi na halmashauri zitumia soko la mitaji badala ya kutegemea bajeti za serikali kupata fedha za miradi.

# Lukuvi amaliza mgogoro ardhi kati ya wanakijiji, mwekezaji

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amemaliza mgogoro wa ardhi kati ya mwekezaji, kampuni ya Dimara na wakazi wa kijiji cha Kisabi uliodumu kwa zaidi ya miaka saba.

Waziri Lukuvi amemaliza mgogoro huo akiwa katika ziara kwenye maeneo yenye migogoro ya ardhi katika mkoa wa Pwani.

Akiwa katika kijiji hicho, Lukuvi alitoa maelekezo ya wavamizi wote waliojimilikisha sehemu ya eneo hilo kuondolewa na kupewa eneo katika shamba la ekari 51 lililorudishwa serikalini hivi karibuni.

Lukuvi alitoa maelekezo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha kufufua mipaka ya eneo hilo na kuweka katika matumizi mazuri ya ardhi, kupima viwanja na kuviuza kwa kushirikiana na mmiliki.

Waziri huyo alisema hayuko tayari kuwavumilia wavamizi kwenye maeneo yanayomilikiwa kihalali. "Nimeamua kuja Pwani kwa kuwa mnaongoza kwa kuvamia maeneo bila kufuata sheria. Kazi yangu ni kuwalinda wanaomiliki ardhi kisheria na kimila. Nataka nirudishe heshima," alisema.

Lukuvi alisema wananchi hao watapewa maeneo kwenye ekari 51 za shamba ambalo lilifutwa umiliki wake na Rais na kurudishwa serikalini na wanalazimika kulipa gharama za hati miliki baada ya viwanja kupimwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha.

Waziri Lukuvi pia aliwaagiza wakuu wa mikoa na wilaya kutembelea maeneo yenye migogoro ya ardhi na kuondoa wavamizi ili kukomesha tabia hiyo. Alitoa onyo kwa maofisa ardhi kuhakikisha wanapopeleka majina ya maeneo ambayo hayajaendelezwa kwa Waziri watende haki kwa kuwa na ushahidi kutoka kwa mkuu wa wilaya atakayekiuka hatua zitachukuliwa.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Aboubakar Kunenge, alizindua kampeni ya kutokomeza migogoro ya ardhi mapema wiki hii lengo kumaliza migogoro iliyopo na kukomesha uvamizi kwenye maeneo yanayomilikiwa kisheria katika mkoa huo.

## Shirika la Bima Zanzibar kujipanua kupitia TPC

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SHIRIKA la Bima la Zanzibar (ZIC) limeingia makubaliano ya kiutendaji na Shirika la Posta nchini (TPC) ili kupanua wigo wa kiutendaji, kuongeza ufanisi wa huduma zake sambamba na kurahisisha upatikanaji wa huduma za kibima hasa maeneo ya vijijini.

Uamuzi huo ulioungwa mkono na serikali kupitia Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar, Dk. Juma Malik Akili, ambaye alisema utasaidia kuongeza mapato kwa mashirika hayo yote mawili, huku akitoa wito kwa mashirika na taasisi mbalimbali za serikali zilizopo Tanzania Bara na Zanzibar kuanzisha mahusiano ya kiutendaji ili kuongeza wigo wa utoaji huduma zao kwa pande zote mbili za nchi.

Akizungumza katika hafla ya kusaini makubaliano hayo jana mjini Zanzibar, Dk. Akili alisema kupitia makubaliano ya namna hiyo wadau wanakuwa kwenye nafasi nzuri ya kupunguza gharama za uendeshaji, kutanua wigo wa huduma na hivyo kuongeza kipato.

Aliyataka mashirika hayo kuhakikisha yanakuwa na utaratibu wa kujifanyia tathmini kila mwaka ili kujua ufanisi wa muungano huo, huku akisisitiza kuwa serikali itakuwa bega kwa bega nayo kuhakikisha ushirikiano huo hauvunjiki na zaidi unakuwa chachu ya kuvutia mashirika mengine kuwa na mahusiano kama hayo ya kibiashara.

Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Amour Hamil Bakari, alimhakikishia Dk. Akili kuwa serikali imejipanga kuhakikisha inalinda kwa nguvu zote uhusiano huo huku ikiendelea kuhamasisha taasisi na mashirika mengine kuiga mfano huo.

Mkurugenzi Mkuu wa ZIC, Arafat Haji na Kaimu Posta Master Mkuu, Macrice Mbodo, waliyataja maeneo makuu matatu yanayohusishwa katika ushirikiano huo ni Shirika la Posta kuwa wakala wa ZIC, Shirika la Bima Zanzibar kutumia huduma za Shirika la Posta hususan katika utumaji wa nyaraka, vipeto, barua na vifurushi pamoja na kutazama na kutumia fursa zilizopo baina ya pande hizo mbili ikiwamo huduma ya rasilimali za majengo na ardhi.

"Kupitia ushirikiano huu, zipo huduma za Shirika la Bima la Zanzibar zitakazotumiwa na Shirika la Posta ikiwamo Huduma ya Bima kwa mali za Shirika la Posta zikiwamo vyombo vya moto na majengo. Tafsiri ya hiki tulichokifanya hapa ni kwamba popote lilipo Shirika la Posta ifahamike pia kuwa hapo pia sisi Shirika la Bima Zanzibar tupo," alisema Arafat.

Mbodo alisisitiza kuwa ushirikiano huo utakuwa na tija zaidi kwa pande zote husussani kipindi ambacho Shirika la Posta lenye matawi yake zaidi 350 nchi nzima pia limewekeza zaidi katika huduma za kidigitali.

# PM aipa kongole Benki ya Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameishukuru Benki ya Afrika (BoA) kwa jitihada zake za kuendelea kuisaidia Tanzania katika sekta mbalimbali za maendeleo.

Majaliwa alitoa shukrani hizo juzi alipozungumza na Rais wa Benki hiyo, Othman Benjelloun, kwenye hoteli ya Sofitel, Rabat nchini Morocco.

Taarifa iliyotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu ilimkariri Majaliwa akisema uwapo wa benki hiyo nchini, umewawezesha wananchi kunufaika na huduma mbalimbali za kifedha.

"Kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, tunaishukuru Benki ya Afrika kwa jitihada hizi," alisema. Waziri Mkuu alimshauri Benjelloun kuendelea kupanua wigo wa huduma za benki hiyo nchini ili kuwafikia Watanzania wengi zaidi hasa katika sekta za elimu, kilimo, mifugo na madini.

Majaliwa, kwa mujibu wa taarifa hiyo, aliahidi kuwa ataandaa utaratibu wa kuukutanisha uongozi wa benki hiyo na sekta binafsi nchini ili kuona namna watakavyoweza kushirikiana katika kuwahudumia Watanzania.

Benjelloun kwa upande wake, alisema lengo la benki hiyo ni kuendelea kukuza uwekezaji wake nchini Tanzania.

"Sisi tuko tayari kuwekeza katika maeneo ambayo viongozi wa taifa la Tanzania watatushauri lengo likiwa ni kutoa mchango wetu katika kujenga uchumi," alisema.

Naye Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, aliiomba benki hiyo isaidie kukuza uhusiano wa Tanzania na Morocco katika sekta ya kilimo hasa kwenye mazao kama mchele, tumbaku na kahawa. Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale wa Zanzibar, Leila Muhamed Mussa, alisema yako maeneo ya fukwe ambayo hayajawekezwa mpaka sasa, hivyo ni fursa kwa wawekezaji kuyatumia na kwamba Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amefungua milango kwa wawekezaji.

Pia aliiomba benki hiyo kuona namna ya kuwawezesha wakulima wa viungo ili kufanya shughuli zao kwa tija.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Masasi, Godffrey Mwambe (kushoto), akipokea msaada wa mabati 460 yenye thamani ya Sh. milioni 17 kutoka kwa Meneja wa Benki ya NMB tawi la Masasi, David Minja, kwa ajili ya kumaliza ukarabati wa shule tatu na zahanati moja za halmashauri ya mji huo, mkoani Mtwara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri ataka watendaji kutatua kero za wananchi

**Na Munir Shemweta,** KONGWA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amewataka watendaji wa ardhi kutoka ofisini na kwenda kusikiliza kero za wananchi katika halmashauri zao ili kuondoa migogoro ya ardhi.

Dk. Mabula alisema hayo juzi wakati akizungumza na wananchi wa Kibaigwa Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma akiwa katika ziara ya kusikiliza na kuzitafutia ufumbuzi kero za ardhi kwenye mikoa ya Morogoro na Dodoma.

Ziara hiyo ya Naibu Waziri ni sehemu ya utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu utatuzi wa migogoro ya ardhi.

Alisema kero nyingi za ardhi katika halmashauri hazihitaji waziri au ngazi ya wizara kwenda kuzitafutia ufumbuzi bali zinaweza kutatuliwa na maofisa ardhi walioko kwenye halmashauri husika.

"Ninachotaka kuona mnatoka kwenda kufanya vikao vya kusikiliza changamoto za ardhi katika halmashauri zenu. Hata kama hakuna kero katoeni elimu watu wajue maana wananchi wanauza ardhi ovyo na hawajui hata mipango ya matumizi ya ardhi. Pia hawajui faida za kupimiwa na kumilikishwa," alisema Dk. Mabula.

Alimtaka Kamishna wa Ardhi Msaidzi Mkoa wa Dodoma, Thadei Kabonge, kuhakikisha anasimamia watendaji wa ardhi kwenye mkoa kutoa elimu ya masuala ya ardhi badala ya kusubiri wananchi kufika ofisini kuwasilisha malalamiko.

Wananchi wa Mji Mdogo wa Kibaigwa wilayani Kongwa waliwasilisha malalamiko yao kwa Naibu Waziri Mabula na kumtaka awasaidie kupata ufumbuzi wa kero zao baada ya kukwama kutatuliwa kwa muda mrefu na maofisa ardhi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa.

Malalamiko mengi yaliyowasilishwa mbele ya Naibu Waziri katika mkutano huo yalikuwa kuhusiana na kudhulumiwa maeneo kwa baadhi ya wananchi, madai ya fidia, uingizaji mifugo kwenye mashamba ya wakulima, ucheleweshaji kesi za ardhi katika mabaraza ya ardhi na kutokamalika kwa urasimishaji kwa baadhi ya maeneo.

Kabonge alisema kupitia mkutano huo wa hadhara kuwa kutokana na kukua kwa mji wa Kibwaigwa, ofisi yake ina mpango wa kuandaa mpango kabambe wa mji huo.

Pia alisema kutokana na kuibuka kwa kero nyingi za ardhi katika mji huo, ofisi yake itakwenda na timu ya wataalamu wa ardhi na Msajili wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ili kusikiliza migogoro ya ardhi na kuipatia ufumbuzi.

HABARI KITAIFA

# Waziri: Shamba la mifugo liendeshwe kibiashara

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, ameagiza uongozi unaosimamia shamba la malisho ya mifugo lililopo Vikuge Wilaya ya Kibaha mkoani Pwani, kujiendesha kibiashara.

Pia ameuagiza kusambaza aina mpya ya mbegu za malisho ijulikanayo kama JUNCAO maeneo mbalimbali nchini kwa kuwa ina sifa ya kustahimili sehemu yenye ukame ili wafugaji wapande malisho hayo.

Ulega alisema hayo alipotembelea na kukagua maendeleo ya shamba hilo na kumwagiza Katibu Mkuu anayeshughulikia Mifugo, Prof. Elisante Ole Gabriel, kuhakikisha aina mpya hiyo ya malisho inasambazwa na kusimamiwa vyema ili ilete tija kwa taifa hususani kwa wafugaji vijijini.

Ulega aliagiza mbegu hiyo ya malisho ya JUNCAO isambazwe kuanzia ngazi ya mikoa, wilaya hadi vijijini, lengo likiwa ni kudhibiti mifugo na wafugaji kuhamahama kutafuta malisho.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha mbegu za malisho hayo zinaenea hadi vijijini kwa wafugaji hususani mikoa yenye ukame kama Dodoma, Singida, Manyara na Shinyanga.

"Kinachosababisha wafugaji kuzunguka na kuhama ni kutafuta malisho na maji kwa ajili ya mifugo yao, hivyo kama watapata mbegu hiyo ya malisho na kuipanda mahali walipo itawasaidia kuwa na uhakika wa malisho hayo na kuacha kuhama hama," alisema Ulega.

Meneja wa shamba hilo la Vikuge, Reuben Ngailo, alisema changamoto wanazokutana nazo katika uendeshaji wa shamba hilo ni kukosekana kwa vifaa na nguvu kazi katika kusafisha shamba na kupanua uzalishaji.

Mbunge wa Chalinze, Ridhiwani Kikwete, aliomba malisho yanayozalishwa shambani hapo kuhakikisha yanawanufaisha pia wakazi wa mkoa wa Pwani.

"Shamba hili lipo kwenye mkoa wa Pwani na ambao una migogoro mingi ya wakulima na wafugaji inayosababishwa na utafutaji wa malisho na maji, hivyo ombi langu ni mbegu hizi zisambazwe haraka kwa wafugaji wa mkoa huu ili itusaidie hata kupunguza migogoro ambayo imekuwa ikitokea baina ya pande hizi mbili za wakulima na wafugaji," alisema Ridhiwani.

## TASAF ilivyonusuru wakulima Pemba

**Na Suleiman Rashid Omar,** PEMBA

NAIBU Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora), Deogratius Ndejembi, ameahidi kuwa serikali zote zitaendelea kuwasaidia maskini ili kuwaondolea ugumu wa maisha.

Aidha, amewataka wanufaika wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), wasitosheke na ruzuku wanayoipata badala yake waanzishe miradi inayowaongezea kipato na kuondokana na utegemezi baada ya muda wa mradi kumalizika.

Naibu Waziri huyo alitoa ahadi hiyo Chakechake baada ya kupokea ripoti ya utekelezaji wa miradi ya TASAF, akiwa katika ziara kisiwani Pemba, kukagua miradi ya mfuko huo.

Alisema lengo ni kuwatoa walengwa kwenye umaskini hivyo serikali kwa kutumia mfuko huo itaendelea kuwapatia ruzuku ili itumiwe kuanzisha miradi ya kuwasaidia sasa na baadaye.

Aliwataka wanaopokea ruzuku kubuni miradi ya maendeleo ya kuwaongezea kipato na TASAF iko tayari kuwasaidia ili kujiendeleza zaidi na kujipatia kipato.

Akikagua ujenzi wa tuta lililozuia maji ya bahari kuingia kwenye mashamba ya wakulima na kuwarejeshea wananchi kulima mpunga, alielezea kuridhishwa na mradi huo na kuipongeza TASAF Pemba kuwa mradi huo una lengo la kuwa ondoshea umaskini wakulima hao.

Ndejembi alitembelea mradi wa ujenzi wa madarasa Gando iliotumia takriban Sh. milioni 71 ambayo sasa yameanza kutumika.

Alisifu kiwango hicho cha fedha ni kidogo kikilinganishwa na ubora na ukubwa madarasa na kusema kuna jambo la kujifunza juu ya ubora na utekelezaji wa miradi ya TASAF kisiwani Pemba.

Alitembelea Kijiji cha Kendwa kwenye kituo cha afya kuangalia kiwanja cha kujengwa hospitali ya kisasa ya eneo hilo ili kuondoa matatizo ya kiafya hasa kwa wajawazito na watoto.

Akiwasilisha ripoti ya utekelezaji, Mratibu wa TASAF Pemba, Mussa Saidi Kisenge, alisema TASAF imetekeleza miradi tofauti ikiwamo kuongeza ajira za muda pamoja na kuvijengea uwezo vikundi vya ushirika .

Alisema kwa upande wa ruzuku, kaya maskini, zimepokea Sh. bilioni 13.8 na sasa wameanza utekelezaji wa awamu ya pili ya TASAF 3, inayoanza na upembuzi yakinifu wa wahitaji na sasa vijiji 24 wamekwishafikiwa.

Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake, Rashid Abdallah Rashid, alishukuru mradi wa TASAF wa kuwajengea tuta wakulima wa shehia ya Ndagoni na kuwaokoa katika kilimo cha mpunga.



Mmoja wa wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa akiukabidhi kwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Ushetu, Elias Kwandikwa, wakati wa makabidhiano baina ya mkoa wa Shinyanga na Tabora, katika Kata ya Kashishi, wilayani Kaliua, mkoani Tabora juzi. **PICHA: NEEMA SAWAKA**

## Watu 71 mbaroni tuhuma za uhalifu

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani linawashikilia watuhumiwa 71 wakiwamo wanawake 20 kwa tuhuma za kuhusika kwenye matukio ya uhalifu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema jana kuwa watuhumiwa hao walikamatwa katika operesheni ya siku 14 iliyofanyika katika wilaya tano za mkoa huo.

Wankyo alisema vitu ambavyo vinadaiwa kuibwa na watuhumiwa hao ni pamoja na sare za Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ(), pikipiki nne, simu 14, televisheni saba, kompyuta mpakato mbili na madumu 35 ya mafuta ya kupikia aina ya MICO Gold.

Vitu vingine vinavyodaiwa kuwa ni vya wizi vilivyokamatwa ni pasi mbili za umeme, visimbuzi viwili, heroin kete nne, mirungi bunda 19, pombe ya moshi (gongo lita 92) na magobole mawili.

Alisema watuhumiwa wote kwa sasa wanashikiliwa na polisi kwa uchunguzi zaidi na watafikishwa mahakamani taratibu zikikamilika.

Kamanda Wankyo amewataka wananchi kutoa ushirikiano wa kuwafichua wahalifu kwenye maeneo yao ili kutokomeza uhalifu katika mkoa huo.

Aidha, alisema jeshi hilo linaendelea kusisitiza kujishughulisha na shughuli za halali za kuwaingizia kipato na kuachana na shughuli haramu ambazo zitawaingiza kwenye mikono ya sheria.

# Waandishi wa habari watakiwa kutokuwa waoga

**Na Christina Mwakangale**

WAANDISHI wa habari wametakiwa kuondoa woga katika kuzitafuta, kuandaa na kuzifikisha kwenye jamii na kuafuata maadili ya kazi, ili kuwapa haki wananchi kuzipata habari.

Hayo yalibainishwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT) kwa kushirikiana na Shirikia la The East African Law Society, wakati wakitoa mafunzo kwa waandishi wa habari 30 kutoka mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Lindi na Mtwara kuhusu uhuru wa habari, yaliyofanyika mkoani hapo.

Kaimu Katibu Mtendaji wa MCT, Ziada Kilobo, alisema jukumu la baraza hilo ni kusimamia weledi na maadili ya kazi na kwamba mazingira rafiki ni muhimu ili kuhakikisha waandishi wanafanya kazi zao vizuri.

"Tunashirikiana na wadau mbalimbali kuhakikisha mnafanya kazi vizuri bila kupata usumbufu wa aina yoyote. East Africa Law Society pamoja na MCT tunajadiliana ili kufikia malengo.

"Mzifahamu sheria, mjifunze mambo gani yanayowakuta katika utekelezaji wenu wa kazi na yanaminya uhuru wa habari na jinsi gani mfanye mkikutana na mazingira hatarishi, kuhakikisha mnaweza kuhabarisha wananchi," alisema Ziada.

"Utabaini kuna wapo waandishi wakienda sehemu wakakosa ushirikiano wakakubali kuondoka kuacha kuchukua habari wakiamini ni changamoto za kazi, bila kujua wamemnyima mwananchi habari," alisema Ziada.

Alisema MCT hufuatilia na kurekodi kila kitu kinachohusisha uminywaji wa taarifa, haki za wanahabari na kwamba baraza kwa kushirikiana na wadau, watatoa msaada wa kisheria kwa waandishi ambao watakutana na kunyanyaswa wakati wakitekeleza haki kwenye majukumu yao.

Meneja Utetezi kutoka Taasisi ya Twaweza, Annastazia Rugaba, alisema takwimu za mwaka 2017 zilionyesha kuwa wananchi waliokwenda kuomba taarifa katika taasisi za umma asilimia 68 walioomba taarifa hawakuzipata.

Alisema licha ya wananchi hao kufuatilia taarifa zaidi ya mara tatu kama utaratibu unavyoelekeza na kwamba taarifa haziwekwi kwenye ubao wa matangazo kwa wakati au kutowekwa kabisa.

Aidha, alisema mbali na taarifa kutafutwa na wananchi, utafiti ikiwamo malalamiko waliyopokea kwenye taasisi hiyo ni kwamba maofisa habari wa taasisi za umma hawana bajeti ya kuandaa taarifa na kutolewa kwa wakati.

"Utakuta ofisa habari katika halmashauri, au ofisi ya umma si mtu wa mwisho kutoa taarifa, utakuta hata DED hatoi taarifa kwa wakati anapofuatwa na waandishi, bila kufahamu haki ni yao kupata taarifa ambazo zinaruhusiwa kisheria kutolewa," alisema Rugaba.

Alisema wanahabari ni kiungo katika kuibua hoja, matatizo mbalimbali ili kupata ufumbuzi wa pamoja ikiwamo hatua zinazopigwa katika kuzitatua, hatimaye kuliletea taifa maendeleo.

"Msiogope, sheria hizi zipo zilipitishwa lakini tunafahamu baadhi zimelalamimiwa kwa sababu zina mapungufu, lakini isiwafanye muogope kusimamia ukweli, weledi, miiko na maadili ya fani yenu, jamii inawahitaji."

Ofisa Mtendaji Mkuu wa East Africa Law Society, Wakili David Sigano, alisema taasisi hiyo inayojumuisha wanasheria wa ukanda wa Afrika Mashariki, itaendelea kushirikiana na wenzao wa Tanzania kuhakikisha sheria zinazolalamikiwa kuminya uhuru wa habari zinapatiwa ufumbuzi.

"Wanahabari mjue tupo pamoja nanyi, katika suala hili," alisema Sigano.

Naye, Wakili Fulgence Massawe akitoa mada kuhusu vyombo vya habari na Uhuru wa Kujieleza, ikizingatiwa sheria na kanuni za hivi karibuni, alisema uandishi wa habari ni zaidi ya taaluma ambayo imeegemea utu na ubinadamu.

"Uandishi wa habari ni zaidi ya utu. Majukumu yao yanakwenda mbali zaidi na kugusa maisha ya mtu moja kwa moja na kutatuliwa ili kuipatia ufumbuzi jamii, kwa kutumia kalamu. Katika jamii yoyote kujieleza ndio haki ya kipekee." Alisema Massawe.




Mkuu wa Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara, Claudia Kitta (aliyevaa gauni la kitenge), akiangalia mashine za kutengeneza mkaa kwa kutumia mazalia ya mazao mbalimbali ikiwamo randa za mbao, maganda ya korosho, maganda ya karanga na vifuu vya nazi wilayani humo jana. **PICHA: HAMISI NASRI**

# Ushindi waichochea WCF kutoa huduma bora

**Na Mwandishi Wetu**

MFUKO wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umepongezwa kwa kuibuka mshindi wa pili katika kundi la Taasisi za Bima na Hifadhi ya Jamii zilizoshiriki kwenye Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya ufungaji wa maonyesho hayo, mmoja wa wadau, alisema ushindi huo ni chachu kwa mfuko kuendelea kutoa huduma nzuri kwa wadau wake ikiwamo kujitangaza kupitia maonyesho na makongamano yanayohusisha wadau tofauti nchini.

"Nawapongeza sana WCF kwa kuibuka washindi wa pili, binafsi niliposikia wapo Sabasaba nilisema ni lazima niwatembelee, na kwa kweli wamenihudumia vizuri sana. Ninashauri wasiishie kushiriki Sabasaba tu, waendelee kujitangaza kupitia makongamano ya wadau, alisema Athuman Saidi, mmoja ya waliotembelea maonyesho hayo.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dk. John Mduma, baada ya kukabidhiwa tuzo hiyo alisema ushindi huo umewapa motisha zaidi kuendelea kutoa huduma za fidia stahiki kwa wakati pamoja na elimu ya taratibu za madai ili kuepukana na vikwazo vinavyochangia mfanyakazi kukosa sifa ya kulipwa fidia yake.

Ameahidi kufanyia kazi maoni yaliyowasilishwa na wadau waliotembelea banda la mfuko huo kwa lengo la kuendelea kuwa mfano wa kuigwa barani Afrika katika utoaji wa huduma za fidia.

"Katika maonyesho haya tumekuwa washindi wa pili kwetu ni wajibu mkubwa tumepewa katika kuonesha tofauti kati ya mshindi na asiyeshinda, lakini zaidi ushindi huu unapaswa kuwa na tija katika utoaji wa huduma za fidia ili kuendelea kuwa mfano wa kuigwa," alisema.

Tuzo hiyo ilitolewa na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, wakati wa sherehe za kufunga maonyesho hayo zilizoenda sambamba na utoaji wa zawadi kwa washindi wa makundi

# Mwambe amwaga mabati, saruji jimboni

**Na Mwandishi Wetu, MTWARA**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Geoffrey Mwambe, ametoa mabati 190 na mifuko ya saruji 260, kwa ajili ya ujenzi wa choo cha walimu, nyumba ya mwalimu na ujenzi wa zahanati wilayani Masasi.

Akizungumza katika ziara aliyoifanya katika vijiji vya Chipole na Machombe kata za Marika na Mumbaka jimboni Masasi, Mwambe, ambaye ni mbunge wa jimbo hilo, alisema lengo la kutoa vitu hivyo ni kusaidia juhudi za serikali katika kutatua changamoto zinazowakabili wananchi wa maeneo hayo.

"Vifaa hivi ni sehemu ya mchango wa juhudi za serikali katika kutatua kero zinazowakabili ili kuboresha mazingira mazuri ya ustawi wa wananchi," alisema Mwambe.

Alisema katika mifuko 260 ya saruji, 100 itatumika katika ujenzi wa choo cha walimu wa Shule ya Msingi Chipole, huku mifuko 160 itatumika katika ujenzi wa Zahanati ya Machombe.

Aidha, alisema bati 30 alizozitoa ni sehemu ya ujenzi wa choo hicho cha walimu na kuahidi zingine 160 kuzitoa siku chache zijazo kwa ajili ya ujenzi wa Zahanati ya Machombe.

# Mradi Barrick sasa kunufaisha wakulima

**Na Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya wakulima 3,000 katika kata za Mwendakulima na Mondo wilayani Kahama, mkoani Shinyanga wamenufaika na mradi wa ujenzi wa kituo cha mafunzo ya kilimo na ufugaji unaofadhiliwa na kampuni ya madini ya Barrick, mgodi wa Buzwagi.

Mradi huo umeanza kunufaisha wakulima, na inaelezwa kuwa kama watatumia ujuzi wanaopata kituoni hapo, watafanikiwa zaidi kwa kuongeza uzalishaji wa mazao na ufugaji wa kisasa.

Hadi sasa mradi huo ambao ulianzishwa mwaka 2018 umeshanufaisha wakulima zaidi ya 3,924 kutoka vijiji 9 katika eneo la Mondo na Mwendakulima.

Akizungumza wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi uliofanywa na Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka huu, Luteni Josephine Mwambashi, Meneja wa mradi huo kutoka Barrick, Elibariki Jambau, alisema mradi unatekelezwa kwa kipindi cha miaka 5 kuanzia mwaka 2018 na utamalizika 2023.

Alisema lengo la mradi ni kuongeza tija kwa mazao ya kilimo na mifugo pamoja na kuwa kitovu cha upatikanaji maarifa ya kilimo na taarifa za masoko ya mazao kutoka kwa wataalamu.

Jambau alisema mpaka mradi kukamilika utagharimu Sh. milioni 529 na hadi sasa kazi zilizokamilika zimegharimu Sh. 138,763,285,00.

Mwambashi, aliipongeza kampuni ya Barrick kwa kuanzisha mradi huo, ambao utanufaisha wakulima wengi na kuwataka wakulima wausimamie uwe endelevu.



Mwajiri bora alivyo na anavyojihadhari dhidi ya sumu tano za mtumishi kazini

Ukurasa 12



BUFE

Ijumaa JULAI 16, 2021

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Ukurasa 14

**Ujue ushirika mikopo wa kinamama TWCC unavyowaweka vifua mbele**

UCHUMI

# Wasomi Tumaini wazuru Tanga wakiwa watalii mafunzoni

- DC kijana awapa nyayo zake, njia ya kutokea

**Na Beatrice Moses, ALIYEKUWA TANGA**

MAFUNZO yoyote yawe ya nadharia au vitendo, ni miongoni mwa mambo muhimu yanayopewa kipaumbele kwenye nyanja mbalimbali, kwa kuwa ni msingi wa mafanikio ya maendeleo kisekta na maisha kiujumla.

Siku ya Juni 25, mwaka huu, wanachuo wa Shahada ya Mawasiliano ya Umma wa Chuo cha Tumaini Dar es Salaam (TUDARCO), walifanya ziara kutembelea baadhi ya vivutio vilivyopo katika mkoa wa Tanga, kujifunza kwa vitendo upigaji picha za habari.

Ni ziara yao iliyowapa fursa ya kumtembelea Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Hashim Mgandiwa, ambaye hakusita kuwasisitiza wasomi hao umuhimu wa kujifunza kwa bidii, ndio mtaji wa mafanikio, pia kulisukuma taifa kimaendeleo kupitia sekta yao ya habari.

Mgandiwa anarejea historia binafsi kwamba, jitihada za kujifunza leo ndiyo zimemfikisha katika uteuzi wa cheo cha sasa, akiwa Tanga, tangu Juni 19 mwaka huu, baada ya kupitia wilaya nne, tofauti zikiwamo Ruangwa na Kigamboni.

"Nyie bado vijana, miongoni mwenu kuna viongozi. Nawasihi dhamana ya uongozi mliyopewa mnapaswa kuwajibika ipasavyo, ili kuendelea kujijengea uaminifu ndani ya chuo.

"Lakini, hata nje ya chuo, hatua ambayo nawahakikisha ipo siku itawanyanyua tena kwenye nafasi nyingine za uongozi wa juu tofauti na mlionao sasa," anasema.

Mgandiwa anasistiza amejijengea uaminifu na uwajibikaji kupitia uongozi, hatua anayoamini imemwezesha kumfikisha alipo sasa.



Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Hashim Mgandilwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Ziara ya Mafunzo, ambaye ni Rais wa Chama cha Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Tumaini, Wilfred John. **PICHA: BEATRECE MOSES**

**UTALII TANGA**

"Tanga kuna vivutio vingi naamini licha ya kwamba mmekuja kujifunza, pia mtakuwa mabalozi wazuri wa kuvitangaza vivutio hivyo kwa kalamu na kamera zenu, pia kuhamasisha utalii wa ndani miongoni mwa wananchi, wakiwamo vijana ambao wengi hufanya vitu kutokana na kuhamasishwa," anasema.

Mgandilwa anadokeza udhaifu wa anaoshuhudia kuwapo vijana wanaosubiri kufuatwa kwa ajili ya frusa mbalimbali, ikiwamo mikopo ya vikundi, ambazo wengi kutokana na kukosa dhamana hawakopesheki, lakini sasa kuna vikundi vinakopesheka, pia wakipewa zawadi ya elimu ya ujasiriamali.

"Pamoja na masomo yenu nawasihi, pia msikwepe kujifunza ujasiriamali mbalimbali utawasaidia na kuwasaidia vijana wengine. Msisite kuwafuata na kuzungumza nao

"Mimi kuna wakati hulazimika kuwafuata kwenye maeneo mbalimbali ninayojua wanapatikana ikiwamo hata disko, wananielewa," anaeleza Mkuu wa Wilaya.

**WENYEWE WAJIELEZA**

Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Ziara ya wanafunzi hao, Wilfred John, ambaye ni Rais wa Serikali ya Wanafunnzi chuoni hapo (TUSODARCO), anakiri wamepokea anayobainisha yamewajenga, naye akimpongeza kuwa katika orodha wateule wakuu wa wilaya vijana.

Anakiri sifa ya wakuu wilaya wahitimu wa chuoni kwao TUDARCO na wamebaki mfano mzuri kwao, ni pamoja na Fatma Nyangasa, Abdallah Mwaipaya, Jerry Murro, Halima Bulembo, Peter Lijualikali na Godwin Gondwe, ambaye pia baadaye alikuwa Mhadhiri Msaidizi.

Ni ziara iliyobeba watu 102, wanajumuishwa na wanafunzi 94, mwalimu wa somo, madereva wanne na wasimamizi wa usafiri wawili.

Wilfred anaitaja kuwa ziara ya mafanikio, kwamba licha ya dharura ambayo hawakutarajia walichelewa na kufika katika Hifadhi ya Amani Wilaya ya Muheza kwenye milima ya Usambara mkoani Tanga usiku, walishuhudia mambo kadhaa na wakaondoka usiku huo kwenda kulala jijini Tanga.

Anataja walishuhudia wadudu kama vinyonga wanaobadilika rangi, huku wasiyoyaona yanajumuisha wadudu jamii ya vipepeo na maporomoko ya maji.

Wilfred anasema siku iliyofuata, ndio walimtembelea Mkuu wa Wilaya ya Tanga, kisha kwenda kwenye Mapango ya Amboni, yanayobeba vivutio vya kihistoria, kisha wakazuru Kituo cha Radio, Wambao FM, ikiwamo katika chumba chake cha studio za matangazo.

Mwanakamati wa ziara na Katibu Mkuu wa TUSODARCO, Glory Olomi, anaeleza lengo kuu la ziara ilikuwa kujifunza somo la habari picha katika maneeo mbalimbali yanayoeleza habari.

"Tulipewa kazi ya kwenda kufanya katika ziara na tuliifanya kwa ufanisi, pamoja na lengo hilo kulikuwa na malengo mengine kama," anasema Glory.

Anaendelea: "Kuona na kujifunza utamaduni wa sehemu nyingine, kukuza mtandao wetu wa watu kwa kutengeneza uhusiano mpya wenye tija, kubadilisha mazingira, kuboresha uhusiano mzuri baina yetu, pia kufurahi na kupumzika."

Mhadhiri Msaidizi wa TURDACO, Ajuaye Mgedela, anayefundisha somo la Upigaji Picha, anasema mafunzo kwa vitendo ni muhimu mithili ya nadharia, kwa kuwajengea uwezo wanafunzi hao, ikiwamo katika aina nyingi za picha.

"Kuna aina nyingi za picha ikiwamo za safari. Maeneo ya utalii kama vile mapango na nyingine nyingi, pia katika ziara hii wanajifunza mazingira na mwonekano wake kulingana na eneo husika," anasema.

# Mwajiri bora alivyo na anavyojihadhari dhidi ya sumu tano za mtumishi kazini

**Na Ummy Matinde, TSJ**

NINI maana ya kazi? Kamusi inataja kuwa shughuli afanyao mtu. Pia, kutoka tafsiri ya kitaalamu, inaenda mbali kwamba, pale nguvu ya binadamu inapotumika katika kutimiza lengo lenye matokeo fulani.

Katika utekezaji wake wa kusaka matokeo ya lengo tajwa, mara nyingi upatikanaji wa jukumu la kufanya kazi hiyo, ambayo ni ajira, nayo ina tatizo lake.

Ili kuajiriwa, mara nyingi anatakiwa awe na dhifa inayofanana na elimu na ujuzi, ili apate sifa ya kumudu kazi, ni bahati mbaya maeneo mengi duniani, wengi wana sifa na wahitahji, lakini fursa za kuajiriwa ni ndogo sana, hata wengi wanabaki mtaani bila ya cha kufanya.

Pia katika walioajiriwa kuna uhaba wa wafanyakazi wenye sifa stahiki. Inapopimwa sifa, kuna wanaobainika na kasoro binafsi kutimiza sifa za kazini.

Hapo kuna kundi la kwanza, waajiri wanaosumbuliwa na wafanyakazi, hata watumishi hao wanaangukia kundi liitwalo 'watumshi mizigo.' Ni wakati huo huo, mtumishi huyo anasaka mafanikio kazini.

Sasa ni namna gani mwajiri anaepuka madhila au tabia hasi kutoka kwa mwajiriwa? Ni wajibu wa mwajiri, awee mjasiriamali, mwenye kampuni au zaidi ya hapo anapaswa kupitia





Namna ilivyo watumishi wakiwajibika katika sehemu za kazi. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

### VIKWAZO VIKUU

Mosi, kuna ulingo wa usambazaji majungu katika maeneo ya kazi; Kimsingi ni sumu kubwa kwenye eneo la kazi na watu wakishaanza kutoleana kauli zisizofaa, mara moja inaharibu uhusiano, ambao hasa ndio mtaji muhimu mahali hapo.

Ni namna inayopomtezea mwenye wasifu wa msingi elimu na stadi, kwani tabia yake inaua mwenendo bora wa uhusiano mahali pa kazi na tija inatoweka.

Hivyo, inatajwa dawa sahihi dhidi ya mwajiriwa ni kumchukulia hatua za kinidhamu, sheria na hata ushauri nasaha ili kuweza kuondoa walakini huo mahali hapo.

Makali ya sumu hiyo ya uhusiano, katika msingi wake inakuwa mbaya zaidi katika zama zilizopo za utandawazi, kwa maana kila jambo linasambaa kwa kasi kubwa hata kuleta adha ya uhusiano kubomoka.

Mbadala unaobaki ni itikadi ya kufanya kazi kwa timu kati ya watumishi wa sehemu moja.

Pili, ni kasoro ya mtumishi anayekumbatia tabia ya kulalamika pasipoisha: Hiyo nayo inatajwa kuwa simu nyingine katika sehemu ya kazi, kwa mfanyakazi badala ya kujenga nyendo ya kujitahidi kusaka majibu yenye ufumbuzi katika mazingira yake binfasi na yanayomzunguka, anaisukuma katika kulalamika.

Sura ya malalamiko hayo huwa ni pana, mathalan wanapompangia majukumu na katika maeneo fulani, wanaangushia majibu ya kulalamika kama ndio sura kuu ya ufumbuzi kwao.

Katika hilo, huwa katika sehemu nyingi kunaelemewa na wapo wanabeba tafsiri ya kuonewa, huku wenza katika sehemu hiyo wanapendelewa kwa gharama zao. Kila kilicho kibaya kwao, hurejesha katika tafsiri ya malalamiko ya kuonewa. Vyote vinajaza sumu katika eneo husika la kazi.

Tiba yake nayo inaangukia sura ya awali, katika taratibu na kanuni rasmi za kazi kama usdhauri nasaha, sheria ma mwongozo husika, ingawaje nako kuna busara na kanuni za kibinadamu ambazio haziko katika sheria zinaweza kutumika.

Ushauri wa jumla kutoka maeneo mbalimbali kitaalamu unabeba sura ya mwajiriwa kujitahidi kujiongezea thamani kwenye eneo lake la kazi, akifuata kanuni na taratibu zilizoko, kwani asiporidhika na fursa ya kuacha kazi, awe na uhuru wa kuelekea kwenye mbadala wake.

Tatu, kuna linalohusu usimamizi wa moja kwa moja kazini: Ni mantiki ambayo kwa wafanyakazi wanaoyajua majukumu yao, wanayatekeleza kwa wakati na kwa ufanisi, daima ni wale wanaliongezea thamani kubwa kwenye kazi wanazofanya.

Kinyume chake, wafanyakazi sumu wana tabia ya kuhitaji usimamizi wa moja kwa moja ndio waweze kutekeleza majukumu yao wanayopewa. Wakiachiwa wabaki katika shughuli zao wawajibike wenyewe, wanakosa uwezo huo. Hulka yao ni mpaka wasimamiwe na wakati mwingine wanatishiwa mithili ya watoto.

Mwajiri katika nafasi yake na hasa kama ni mjasiriamali anayepigana kuibuka, hukosa muda wa kutosha kuanza kumsimamia kila mfanyakazi kwa anachofanya, hivyo wafanyakazi anapokuwapo wa aina hiyo, wanabaki kuwa mzigo mkuu kwa mwelezaji.

Uwajibika binafsi wa mtumishi katika eneo lake la kazi, ni msaada mkubwa kwa msimamizi kupata muda mbadala wa kusimamia mengine ambayo yana nafasi ya kuuinua zaidi mradi.

Kinyume chake, mtumishi akiwa katika hulka inayomfanya mwajiri anakesha katika usimamizi wa mfanyakazi muda wote, tayari huyo anakuwa mzigo ulio tatizo kwa mwajiri namaendeleo ya uwekezaji kwea ujumla.

Hapo pia kuna la ziada, mwajiri anapaswa kujifunza zairo kuongoza, naye akijiongoza kwa mambo kupitia nyenzio kama vile kupanga ratiba binafsi, kuzifuata, kuyajua majukymu yake ya msingi na namna ya kuyatekeleza kwa wakati na ufanisi.

Nne, kuna sura ya vikwazo kazini katika ya kuyajua majukumu binafsi: Ni mtazamo unaoanza na umuhimu katika kusimama katika imani kwamba hakuna mtu asiyekosea kazini, kwani ukweli uko katika kinyume chake kila binadamu anakosea.

Si sahihi mtu akaondolewa kazini, kwa dai la kukosea, lakini kuna ukwerli uluiinjificha kwamba, aliyekosea anakataa ukweli wa jambo hilo.

Hiyo inaangukia kuwa sumu, kwa sababu ni kuficha kasoro na kutotoa fursa ya kujifunza na 'kulikoni kwenye chanzo' na nafasi ya kujirekebisha kupitia ushuhuda.

Mwajiri, katik ahili anaye wajibu wa kulielewesha kwa kina, katika namna ya kudhibiti kasoro, hapo ndipo yanapoonekana endelevu katika stahiki kazini za nidhamu, sheria na maonyo inachukua nafasi.

Ili kubaki salama, nasaha kwa mwajiriwa, anapaswa kuhakikisha anayajua majukumu yake vyema na anayeyatekeleza kwa ubora wa hali ya juu, kwa kiwango cha utendaji wake na anapokosea akubali, kujenga mlango wa marekebisho.

Tano, kuna angalizo la anapoonekana mfanyakazi anachoangalia ni fedha tu bila ya kazi na sheria, ni 'sumu yenye bomu' iliyo hatarini kumwangukia mwenyewe;

Pale mfanyakazi anapojikita katika kuhubiri kifikra, pasipo ubora na nidhamu ya kazi, inageuka kuwa sumu aina yake na mara zote, uzoefu unaanika watumishi wa namna hiyo, wana mwenendo 'unaopishana mlangoni na ubora wa kazi."

Kwa mwajiri, mara anapoiona sumu ya aina hiyo katika sehemu yake ya kazi, naye anapaswa kuchukua hatua stahiki kudhibiti kabla haijachukua sura ya janga dhidi yake na taasisi anayoisimamia. Ikiwa hali ni mbaya zaidi, inawasha kiashiria cha kuachana na mwajiriwa huyo.

Darasa la nasaha, ni kwamba kabla hajatafakari ya pesa za ziada kutoka ulingoni mwa mwajiri, ana wajibu wa kujiuliza uhalali wake na tafakuri ya "Nimemfanyia nini mwajiri, kabla mimi sijaanza kumdai."

### SIFA ENEO LA KAZI

Wasifu wa eneo la kazi unatajwa kwamba unapaswa kuwa sehemu ambayo watu wanafurahia kuwapo na wanashirikiana, ili kutoa bidhaa au huduma inayowasaidia wateja wa kazi husika.

Kama kuna mfanyakazi yeyote anayekuwa kikwazo kwenye mchakato huo, anabeba sifa ya 'sumu' na ananayohitaji tiba.

Pia, suala la ushirikiano kati ya mwajiri, mwajiriwa na wafanyakazi kwa ujumla, unahitaji kuwa na sura pana hiyo ndio inazaa majibu chanya yaliyopangwa, mbele ya utekelezaji ulio na milima na mabonde.


Kwa ujumla, wajibu wa kila mmoja kuchukua hatua kwa pale anapohusika na mambo yatakuwa majibu yanakuwa mazuri, kama ambavyo Hayati Rais Julius Nyerere mwaka 1964 alivyotamka kwa nukuu ya Kiingereza 'It can be done, play your part' kwa maana ya yote yanawezekana, timiza wajibu wako.

- ***Makala hii imeandaliwa kwa msaada wa taarifa za uchambuzi fani ya rasilimali watu. Mwandishi anapatikana kupitia namba 0673686195 au barua pepe; ummyodilia@gmail.com***

---

## TAFAKURI YA MLALAHOI

# Zimamoto wasigeuzwe yatima




**Na Joseph Kulangwa**

MOTO una pande mbili, upande mzuri na mbaya. Mzuri ni pale unapotumika kupasha joto palipo na baridi na kuwezesha watu kukaa sawa miilini.

Upande mzuri ni pale unapotumika kupikia chakula, jambo ambalo ni muhimu kwa maisha ya binadamu. Kukosa chakula maana yake ni kudhoofisha mwili.

Lakini, upande mbaya ni pale moto unapounguza mwili, unapounguza mali, unaposababisha uharibifu kwa jamii. Hata katika vitabu vya dini, inasemekana moto ndiyo adhabu ya juu kabisa kwa wenye dhambi.

Hapo ndipo moto unapochukuliwa kama laana kwa binadamu na kuwa kitu kisichotakiwa kabisa katika jamii. Zipo semi kwamba 'usicheze na moto utaungua.'

Kama kuna kundi ninalihurumia sana nchini, ni la wazima moto, mara nyingine huitwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, wakati mwingine huitwa Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji.

Tuite tu ni Jeshi kwa sababu linaongozwa na Kamishna Jenerali kama ilivyo kwa Jeshi la Magereza na lilishapewa hadhi hiyo rasmi.

Lakini, kwa kuwa jeshi, nadhani ama halina wapiganaji wazuri au zana nzuri za kukabiliana na adui ajali ikiwamo ya moto. Ndiyo sababu utasikia, moto umeteketeza mahali na zimamoto wamefika ama wamechelewa au bila maji.

Mfano mzuri ni wa hivi karibuni, soko kuu la kimataifa la Kariakoo liliposhika moto na kuteketeza sehemu yake kubwa. Zimamoto walioko karibu kabisa na eneo hilo, wakafika lakini bila maji ya kutosha.

Kamishna Jenerali John Misungwi, akawaambia



**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: jkulangwa@yahoo.com

Watanzania waliomkabidhi majukumu ya kuzima moto na kufanya uokoaji wa maisha na mali, kwamba waliishiwa maji, hivyo kulazimika kiyafuata uliko Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere. Kilomita inazidi kidogo 10 kutoka Kariakoo,

Mtu aendeshe gari kubwa, lori la maji, kutoka Kariakoo hadi uwanja wa ndege na kurudi, takriban kilometa 20, bado muda wa kujaza maji, huo moto utakuwa unamsubiri? Si rahisi haiwezekani kabisa!

Kama haitoshi, Misungwi akaongeza, kwamba hata humo njiani walimokuwa wakipita kwenda kuzima moto huo, wakakumbana na changamoto ya watu kuziba njia wakifurika kushuhudia.

Kwa Wabongo sishangai, kwa sababu wamezoea kushangaa kila kitu kinapotokea. Wakisikia mabomu yamelipuka mahali, watakimbilia kushuhudia. Mnakumbuka enzi za Gongo la Mboto na Mbagala, walivyokuwa wanakutana nayo njiani?

Lakini Misungwi, si magari yenu yana ving'ora! Yaani huko njiani mkipita, si lazima mpishwe au siku hiyo havikulia, au Wabongo walishachanganyikiwa na kuziba masikio na kutosikia wala kuona vimulimuli vyenu?

Tuyaache hayo, lakini nadhani Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaonewa sana kimiundombinu na hata kizana. Zamani kulikuwa na mifumo ya kuchota maji kwa ajili ya kujaza kwenye magari, pia mifumo hiyo ikizima moto kama iko karibu.

Leo haijulikani ilikoishia, kutokana na ujenzi holela mijini, bila kuthamini umuhimu wa mifumo hiyo na hakuna aliyejali, wakiwamo Zimamoto wenyewe ambao wanapaswa kufuatilia ujenzi mijini na kuzingatia njia za kupita magari yao.

Wakaacha, wakakaa kimya na kushuhudia matajiri wakisimika maghorofa na kuziba njia za magari kupita nyakati za dharura kama hiyo ya Kariakoo, leo yametupata ndipo tunalia, watu wanaziba njia, mifumo haionekani mpaka tunasafiri masafa kufuata maji Uwanja wa Ndege, duh!

Pia, yawezekana Zimamoto kutojua wajibu wao kikamilifu, ndiyo sababu hata baadhi ya majukumu wanaporwa na Jeshi la Polisi. Hivi uokoaji unaanza na kuishia wapi? Angalia zitokeapo ajali za barabarani, nani wanakuwa wa kwanza kufika na kutoa matamko?

Mara zote utamwona Kamanda wa Polisi wa Mkoa wenye tukio, akiwa eneo la tukio, akizungumza na wanahabari badala ya Kamanda wa Zimamoto, ambaye ndiye anahusika na uokoaji!

Polisi kazi yao ni kupima ukubwa na namna ya ajali, na kutafuta kama kuna jinai. Zimamoto waokoe kwanza. Hilo linafanyika?

Zimamoto wasaidiwe kujua majukumu yao, wapewe zana, wakitaka kununua ndege zisizo na marubani kuzimia moto wasiambiwe ni kamera, magari ya kisasa ya kuzima moto ni muhimu kama rasilimali watu. Alamsiki!

BIASHARA

# Ujue ushirika mikopo ya kinamama TWCC unavyowaweka vifua mbele

- Dhamana mtaji, masharti uliowekewa
- Kapata nyumba, maduka 3... ughaibuni

**Na Christina Mwakangale**

KATI ya matatizo ambayo wanawake kwa asilimia kubwa hukumbana nayo katika shughuli za biashara, ni pamoja na kupata mikopo ili kukuza biashara zao.

Kikwazo kilichopo sasa dhamana, kwa sababu mikopo iliyopo kwenye taasisi za kifedha ikiwamo benki, sharti mkopaji awe na hati ya nyumba, mali au ardhi yenye thamani ambayo inakaribia kiwango cha mkopo.

Katika kubaini hilo Chama cha Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (TWCC), kimeanzisha Chama cha Akiba na Mikopo, TWCC-SACCOS, ili kuwapatia mikopo kinamama ambao ni wanachama wa chama hicho bila dhamana kwa masharti nafuu.

Mratibu wa TWCC- SACCOS, Nelson Mbalamwezi, anasema hadi sasa waliopatiwa mkopo ni 35 kati ya wanachama wote 127, tangu kuanzishwa kwa Saccos mwaka 2017.

Anasema, chama hicho kilianzisha baada ya kubainika kinamama wengi wanashindwa kuanzisha au kuendeleza biashara zao, kwa kukosa vigezo vya kukopa kwa kuwa hawamiliki nyumba, hati, ardhi hata mali.

"Kama inavyofahamika mwanamke anayemiliki nyumba na hati kwa familia za kiafrika ni nadra, mara nyingi baba ndiye mmiliki. Tukaona hivi sasa wanawake wengi wapo kwenye ujasiriamali na wanalisha familia zao kuliko hata kinababa, tukaona tumsaidie kumuinua kiuchumi mama huyu," anasema Mbalamwezi.

Kuhusu ukopaji, Mbalamwezi anasema, mkopaji huhitaji akiba na idadi ya hisa za kutosha katika katika 'SACCOS' hiyo na kudhaminiwa na mwanachama mwenzake, pasipo kujali ama hati au mali, akisema dhamana kubwa sio kipaumbele kwao.

"Kiwango cha mkopo kinaanzia kati na Sh. 60,000 hadi milioni 10. Huu ni mkopo wa mtu mmoja mmoja, kurudisha ni kwa kipindi cha miezi 12 na marejesho la kila mwezi, itatokana na hesabu ya mkopo wako. Kabla ya kukopeshwa huwa tunamfanyia mapitio mkopaji kwa kuangalia eneo lake la biashara na kumshauri," anasema mratibu huyo.

Anabainisha walio na vigezo vya kuwa mwanachama wa TWCC ni kwa yeyote na kwamba ni ruhusa kujiunga na chama kwa kuegemea kundi lolote kati ya manne yaliyopo kwenye chama hicho ambayo ni mwanchama binafsi, kampuni, kikundi na jumuiya.

Anasema makundi hayo viingilio vyao hutokana na vigezo kadhaa vilivyowekwa kulingana na utaratibu wa chama, akianzia kiingilio cha kampuni, kikundi ni Sh. 100,000 na wanapaswa kulipa ada ya Sh. 50,000 na ununuzi wa hisa ni namna walivyojipanga na moja huuzwa wastani wa Sh. 100,000.

Mbalamwezi anasema kiingilio cha Saccos kwa mwanachama wa TWCC, ni Sh. 100,000 na kwamba akiba ya kila mwezi ni Sh. 30,000 huku hisa moja ikiuzwa Sh. 100,000.



Rehema Patrick, mjasiriamali kutoka mkoani Morogoro, akionyesha bidhaa zake aliposhiriki Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba, yaliyofanyika mwaka huu kuanzia Juni 28 hadi Julai 13. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

> **"Kinamama wajishughulishe, wasikate tamaa watainuka. Mfano mimi bidhaa zangu nauza bei ya kawaida tu kiungo kimoja ni kati ya Sh. 3,000 hadi 5,000 kulingana na ujazo**

"Sababu ya kuanzisha Saccos hii ni kutoa huduma ya kifedha kwa wanawake, kwa urahisi. Kwanza, wanawake wana changomoto ya kupata mkopo mara nyingi hawana hati, ardhi mali ambayo ni dhamana kila wakitaka kukopa katika benki," anasema.

### SACCOS YENYEWE

Mblamwezi anasema kwamba TWCC SACCOS, ni asasi ndogo ya kifedha kwa lengo la kuwahudumia wanachama wake kwa kuwapatia huduma mbalimbali za kifedha ili kukidhi mahitaji ya kiuchumi, kijamii na ya kimazingira kwa kufuata misingi ya ushirika, kanuni za vyama vya ushirika, Sheria ya Vyama vya Ushirika pamoja na masharti ya chama.

"Dhamira ni kuinua, kustawisha na kuboresha hali ya kiuchumi na kijamii kama majukumu yake ya asili ya ushirika kwa wanachama, kwa kuhamasisha kuweka akiba zenye utoshelev u na kuwapatia mikopo yenye masharti na riba nafuu," anasema Mbalamwezi.

Anabainisha kwamba kaulimbiu ya 'SACCOS' hiyo inasema: 'Kushirikiana na mwanamke mjasiriamali kutimiza ndoto yake," ikiwapatia kinamama mikopo, fursa ya uwekezaji hisa, akiba, pamoja na taarifa za masoko.

"Kwa kuzingatia kaulimbiu yetu ya kushirikiana na mjasiriamali kutimiza ndoto yake, Saccos inatoa mikopo kwa riba ya asilimia 10 tu (flat rate) na masharti nafuu. Hadi sasa, kwa wanachama wote waliokidhi vigezo na kuomba mkopo wamenufaika." Anafafanua.

### SHUHUDA MNUFAIKA

Rehema Patrick, ni mjasiriamali aliyekuza biashara yake kupitia TWCC SACCOS kwa kupata mkopo na hata kupata fursa ya soko alipodhuru Rwanda.

Rehema mkazi wa Kilakala, mkoani Morogoro anajihusisha na kuuza viungo mbalimbali, ambavyo hutokana na an ayvoitaja; mdalasini, pilipili manga, hiliki, majani ya mimea tiba, viungo vya pilau na kwamba huandaa dawa maalumu kwa wanaosumbuliwa na vidonda vya tumbo.

"Malighafi za viungo hivi hupatikana hapahapa Morogoro, vinalimwa na wakulima na ninakwenda kununua na kuandaa viungo. Kuna wakati nilipata mteja kutoka Falme za Kiarabu, alinunua," anasema.

Anasema alifika jijini Kigali, Rwanda mwaka 2019, kupitia maonyesho yaliyopewa jina la Juakali na kuonyesha bidhaa zake ambazo anazitambulisha kwa jina la 'EDEN Products' akisema biashara haikuwa kubwa sana, lakini alijenga mtandao wa wateja na kujitangaza zaidi.

"Nimeweza kufungua duka la tatu baada ya kukopa Sh. milioni tatu katika SACCOS hii. Nilikopa mwaka jana, nimeboresha biashara na mkopo huu wa miezi 11, umeniinua naiona faida, tumejenga nyumba na mume wangu na tumefanikiwa kusomesha watoto wetu wawili chuo kikuu.

"Mkopo umeniimarisha nami nimeajiri wafanyakazi nawalipa mshahara watu wasiopungua watano, na nina wakala wa bidhaa hizi katika mikoa ya Arusha, Dodoma na Dar es Salaam," anasema na kushauri:

"Kinamama wajishughulishe, wasikate tamaa watainuka. Mfano mimi bidhaa zangu nauza bei ya kawaida tu kiungo kimoja ni kati ya Sh. 3,000 hadi 5,000 kulingana ujazo."

### MKURUGENZI TWCC

Mkurugenzi Mkuu wa TWCC, Mwajuma Hamza, anasema wanawake wa chama wananufaika na kuinuka kutokana na kupewa mafuzo mahsusi namna na kuitangaza biashara yake, kuielezea na namna bora ya ufungashaji ili kumvutia mteja.

"Mpangilio wa bidhaa yako, ufungashaji na uijue bidhaa yako na kuilezea ipasavyo ni siri ya mafanikio, sio mteja anahitaji maelezo na manufaa ya bidhaa yako unashindwa kuitambulisha na kuitetea sokoni," anasema Meneja Mwajuma.





# Azaki zatakiwa kuelimisha vijana kilimo na ufugaji

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, amelishauri Baraza la Taifa la Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO) kuwa daraja la kusaidia vijana kuwaelimisha kujitambua na kuchangamkia fursa za kilimo na ufugaji.

Pinda aliyasema hayo alipotembelewa na wajumbe wa baraza hilo nyumbani kwake Zuzu kwa lengo la kujifunza namna alivyowekeza katika sekta ya kilimo na ufugaji.

Alisema vijana wana nafasi kubwa kutoa mchango wa taifa, hivyo wanatakiwa kuchangamikia fursa zinazowazunguka hususan sekta ya kilimo na kubainisha kuwa kuna haja ya kuwa na kituo cha kilimo kila kanda, hali itakayochochea zaidi vijana kujikita kwenye sekta hiyo.

"Kwa takwimu zilizopo, kundi la hawa vijana ni kubwa sana, kikubwa ambacho mnatakiwa kukiangalia ni kuwaangalia hawa vijana kwa mawanda mapana kundi la vijana ambao hawakusoma na vijana wasomi, ukitaka kuwasaidia vijana lazima uangalie unafanyaje," alisema na kuongeza:

"Ushauri wa kwanza tujaribu kuwaasa vijana wajitambue kuwa wao sio taifa la kesho bali ni taifa la leo, yote na yote kama kijana lazima uangalie fursa zinazokuzunguka hivyo ninyi Baraza mnatakiwa muwe daraja la kuwaelimisha vijana wachangamkie fursa hasa kilimo."

Aidha, Pinda aliwaasa kuwa mstari wa mbele katika kuelimisha jamii kuondokana na hali ya utapiamlo nchini pamoja na mapambano dhidi ya umaskini.

Alitoa wito kuwa na uwazi masuala ya kifedha kwa asasi za kiraia ili kuaminika zaidi kwa serikali.

Naye Mwenyekiti wa Baraza hilo, Lilian Badi, alisema hatua ya ziara hiyo wamejifunza mengi kuhusu masuala ya kilimo huku akitoa ombi la kuwezeshwa kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya baraza hilo.

# Kampuni 1,500 za Tanzania kushiriki miradi mikubwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KAMPUNI zaidi ya 1,500 nchini, zimepata nafasi ya kushiriki utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), bwawa la kufufua umeme la Nyerere (JNHPP) na miradi mingine iliyoanzishwa kwenye serikali ya awamu ya tano.

Katibu wa Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Beng'i Issa, alitoa kauli hiyo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya Baraza hilo kuhamia Dodoma.

Alisema pia zaidi ya wananchi 50,000 wamepata ajira katika miradi hiyo inayoendelea kutekelezwa kwenye maeneo mbalimbali.

Beng'i alisema ajira hizo ni sehemu ya mafanikio ya Baraza tangu kuanzishwa kwake miaka 14 iliyopita licha ya kuwapo na vikwazo mbalimbali ambavyo vimeendelea kutatuliwa kwa kushirikiana na wadau.

Akizungumzia utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa katika mkutano wake na wanawake Juni 7 mwaka huu jijini Dodoma ya kuwataka kusimamia haki za wanawake kiuchumi kupitia majukwaa ya wanawake katika ngazi ya mikoa, wilaya na kata yaliyopo nchi nzima, Katibu huyo alisema yote yapo katika utekelezaji.

Alisema licha ya Rais kuahidi kuyalea majukwaa hayo, zipo kero zinazowakabili hivyo baraza lina jukumu la kuhakikisha wanapata taarifa na kuwezesha ofisi ya Rais kupata taarifa za kiutendaji wa majukwaa.

Alisema kwa sasa wamejiandaa kupitia mwongozo wa uendeshaji wa majukwaa hayo na kusimamia utendaji wake kwa kushirikiana wadau mbalimbali ili kufanikisha malengo yaliyokusudiwa.

Aidha, alisema masuala ya mikopo kwa wanawake katika mifuko inayotoa mikopo kwa wanawake bado wanalifanyia kazi ili kuboresha utendaji wa mfuko inayotoa mikopo kwa wananchi wengi hususani wanawake.

Alisema katika kuboresha haki ya kiuchumi kwa wanawake tayari kazi wameshaanza kuifanya.

"Tumeanza kulifanyia kazi ikiwa ni pamoja na kutafuta wadau ambao wanawaza wakafanya nao kazi, kutengeneza jinsi ya kufanya kazi hiyo kama nchi ikizingatiwa kuwa suala hilo ni la kimataifa."

"Kwa sasa yapo majukwaa 23 ngazi ya mkoa yaliyoanzishwa mwaka 2017, majukwaa 144 ngazi ya wilaya, majukwaa 350 ngazi ya kata, majukwaa 514 ngazi ya kijiji," alisema Katibu.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, akizungumza na wananchi wa Mji Mdogo wa Kibaigwa, Wilaya ya Kongwa, mkoani Dodoma wakati wa ziara ya kusikiliza na kuzitafutia ufumbuzi kero za ardhi katika wilaya hiyo jana. Wapili kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Remidius Mwema. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# Walimu wapewa changamoto ya maadili

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT), kimesema kukosekana kwa uaminifu kwa walimu katika kusimamia mitihani ya taifa ni moja ya sababu zilizoilazimu serikali kutumia mgambo na askari polisi kuwasimamia walimu.

Katibu wa CWT, Deus Seif, alibainisha hayo juzi katika Kongamano la Mwalimu wa karne ya 21 la Chama cha Walimu Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOSTA) lililoambatana na sherehe ya kuwaaga wahitimu wa mwaka wa tatu wa ualimu.

Seif alisema kutokana na kuongezeka kwa vitendo hivyo, kuna wakati watapelekewa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kuwasimamia, jambo ambalo ni la aibu kwa kada ya walimu, hivyo ni lazima wabadilishe tabia na mienendo yao.

"Walimu wa karne ya 21 mzingatie maadili

mliopewa shuleni ili msaidie kurejesha nidhamu kama ilivyokuwa miaka ya 80 ambapo mitihani ilisimamiwa na walimu pekee," alisema.

Alisema kitendo cha walimu kukosa uaminifu ni kuvunja maadili, kanuni na miongozo ya utendaji kazi kwa kada hiyo na ni jambo ambalo linawatia doa.

Aliwataka walimu kubadilika na kurejea kwenye miiko ya ualimu na kuachana na tabia ya wizi wa mitihani, ambayo inasababisha hali hiyo.

"Hatujachelewa, muda bado upo tubadilike, turejee kwenye miiko yetu kama tukivyojifunza vyuoni, tutambue kuwa vitendo hivyo pia vimekuwa vikiwanyima haki watoto, kutokana na kuingia hofu wanapoona chumba cha mitihani wamesimamiwa na askari kwenye silaha au mgambo," alisema na kuendelea:

"Tuache jamani, tuwe kama walimu wa miaka 80 ambao walikuwa waaminifu na jukumu la mitihani walisimamie wenyewe."

Kuhusu ajira za walimu, alisema mwaka jana walipeleka ombi kwa aliyekuwa Rais, Hayati, Dk. John Magufuli, ambaye alikubali na

ndio ulikuwa msingi wa walimu zaidi ya nafasi 6,000 za ajira zilizotolewa na serikali hivi karibuni.

Seif alisema CWT itaendelea kuwasilisha ombi hilo kila inapopata nafasi ya kukutana na kuzungumza na serikali na kushauriana katika mambo mbalimbali.

Awali, akisoma risala Katibu Mkuu wa UDOSTA, Emanuel Mwangoka, aliiomba CWT kufikisha pendekezo kwenye uongozi kuendelea kupambana na kushauriana na serikali yao kuhusiana na upatikanaji wa ajira na kutengeneza mazingira rafiki kwa ajili ya vijana kujiajiri, huku wakisubiri utaratibu rasmi wa kuingia kwenye ajira za kudumu kwa wahitimu wa mwaka 2015 hadi 2020.



# Mbeya yakiri kuwapo wagonjwa corona

Na Nebart Msokwa, MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imekiri uwapo wa wagonjwa wa corona wanaoendelea na matibabu katika baadhi ya vituo vilivyotengwa kwa ajili ya ugonjwa huo huku ikiwataka wananchi kuchukua tahadhari za kujikinga zilizoainishwa na wataalamu.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliyasema hayo jana alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusu mikakati ya mkoa huo kukabiliana na janga hilo, bila kutaja takwimu kwa maelezo kuwa hana mamlaka ya kuzitoa kwa mujibu wa sheria.

Homera alisema watu wenye mamlaka ya kutaja takwimu za wagonjwa wa corona ni Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Waziri Mkuu ama Rais.

Kutokana na uwapo wa maambukizi ya ugonjwa huo, Homera aliwaagiza wakuu wa wilaya zote za mkoa huo kwa kushirikiana na Kamati za Afya za Halmashauri, kutoa elimu ya kujikinga kwa wananchi ndani ya siku saba.

Aliwataka viongozi hao kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kuweka mikakati ya kukabili ugonjwa huo ili usienee zaidi kwenye maeneo yao.

Alisema mkoa huo umeainisha mikakati mbalimbali ya kukabiliana na ugonjwa huo ikiwamo kuwataka wananchi kunawa mikono mara kwa mara kwa kutumia maji tiririka na sabuni, kuepuka mikusanyiko isiyokuwa ya lazima na kuvaa barakoa pale wanapolazimika kukusanyika.

Vilevile, aliagiza wanafunzi wa ngazi zote mkoani humo kuanza kuvaa barakoa wanapokuwa shuleni isipokuwa watoto wenye umri wa chini ya miaka minane ambao hawatatakiwa kuvaa isipokuwa taratibu zingine watatakiwa kuzingatia.

"Vilevile tumeagiza vyombo vyote vya usafiri vibebe abiria kulingana na uwezo wake na siyo kujaza abiria kupita kiasi, mtu yeyote anayepanda gari ya abiria lazima avae barakoa na tumeelekeza maeneo yote ya vituo vya mabasi kuwa na ndoo za kunawia," alisema Homera na kuongeza.

"Pia tumeelekeza maeneo yote ya mikusanyiko ikiwamo baa, makanisani na misikitini, watu wavae barakoa na nje ziwekwe ndoo za maji kwa ajili ya watu kunawa kabla hawajaingia na wakifika huko wasikae kwa kukaribiana," alisema Homera.

Aliwataka wananchi wote watakaojihisi kuwa na dalili za ugonjwa huo ikiwamo kujisikia homa kali, mafua makali, kushindwa kupumua vizuri, kukosa hamu ya kula na uwezo wa kunusa kwenda katika vituo vya kutolea huduma za afya ili wapate matibabu.

Pia, alionya wananchi kujificha majumbani wanapohisi dalili za ugonjwa huo kwa kuwa unatibika kwa urahisi zaidi mtu anapowahi hospitalini.

Homera alisema vimetengwa vituo mbalimbali ndani ya mkoa huo kwa ajili ya matibabu ya wagonjwa wa corona ikiwamo katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya, Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya pamoja na halmashauri zote vilipotengwa vituo.

Kwa upande wao baadhi ya wakuu wa wilaya za Mkoa wa Mbeya, waliwataka wananchi kuchukuta tahadhari bila kusubiri kulazimishwa na serikali kwa sababu madhara ya ugonjwa huo ni makubwa.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune aliwataka wananchi kuziamini taarifa zinazotolewa na viongozi wa serikali na taarifa hizo ni rasmi.



Naibu Spika na Mbunge wa Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson, akizungumza na madereva pikipiki na bajaji wa Jiji la Mbeya juzi, wakati wa kuhitimisha mafunzo maalumu kwa madereva hao kuhusu sheria za usalama barabarani, ambapo zaidi ya vijana 100 walihudhuria. Kulia kwake ni Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Wilbroad Mutafungwa. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Chanzo cha ajali kwa madereva chaelezwa

Na Nebart Msokwa, MBEYA

KUTOPATA muda wa kupumzika na kuendekeza ngono kwa baadhi ya madereva wa mabasi ya masafa marefu ndiyo chanzo cha ajali nyingi za barababani.

Hayo yalisemwa juzi na Ofisa Mkaguzi wa magari wa Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Mbeya, Yusuph Masoli, wakati wa kikao maalumu kati ya Jeshi la Polisi na wadau wa usafirishaji kilicholenga kuweka mikakati ya kukabiliana na ajali za barabarani.

Alisema baadhi ya madereva wakishafika safari zao huwa hawapati muda wa kupumzika na badala yake wanaingia kwenye maeneo ya starehe ambako wanalewa kupita kiasi na baadhi yao kulala na wanawake na kutopumzika vizuri hali inayowaongezea uchovu.

Alisema madereva wa aina hiyo wakianza kuendesha magari asubuhi kunakuwa na uwezekano mkubwa wa kusababisha ajali kwa sababu unafika muda wanakuwa wanaendesha magari huku wakisinzia.

"Dereva unakaa bara mpaka saa saba au saa nane usiku unalewa na ikiwezekana unachukua na mwanamke unaenda kulala naye halafu saa 12 asubuhi unaanza kuendesha gari huku ukiwa bado una usingizi, hii ni hatari kwa sababu unaweza ukasinzia wakati unaendesha na ukasababisha ajali," alisema Masoli.

Naye mwalimu wa masuala ya usalama barabarani kutoka katika Ofisi ya Mkuu wa Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Mbeya, Joseph Mwamalumbila, alisema baadhi ya magari yanayofanya safari kati ya Mkoa huo na mikoa mingine ni mabovu.

Aliyataja mabasi hayo kuwa ni yale yanayofanya safari kati ya Mbeya na Tabora na Mbeya na Mwanza huku akidai kuwa baadhi ya mabasi hayo huwa yanajaza abiria kupita kiasi.

Aliwataka abiria wote wa mabasi kuhakikisha wanapopanda kwenye magari wafunge mikanda ili kuepuka kupata madhara makubwa pale inapotokea ajali.

# Kampuni yaagizwa kuwarahisishia wakulima teknolojia

Na Nebart Msokwa, MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imeitaka Kampuni ya Mbolea ya Yara, kuhakikisha programu mpya ya YaraConnect inayotoa elimu ya utaalamu wa kilimo kwa njia ya kidigitali kwa ajili ya wauzaji wa pembejeo za kilimo kuwa rahisi kutumiwa na wakulima ili ilete matokeo chanya.

Mkuu wa Mkoa huo, Juma Homera alitoa ushauri huo juzi kupitia hotuba yake iliyosomwa kwa niaba yake na Katibu Tawala Msaidizi, Uchumi na Uzalishaji, Said Maditto, wakati wa uzinduzi wa programu hiyo ambayo itawasaidia mawakala wa kampuni hiyo kuuza pembejeo kwa njia ya kielektroniki.

Alisema endapo wakulima watawezeshwa kuitumia programu hiyo itawasaidia kupata elimu moja kwa moja kutoka Yara kuhusu matumizi sahihi ya mbolea wanayonunua kutoka kwa wauzaji jambo litakalosaidia kuwapa ufanisi kwa haraka.

"Wakulima wakiwezeshwa kuwasiliana moja kwa moja na Yara itasaidia kutatua matatizo yao na kupata maelezo ya moja kwa moja kuhusu ufanisi ama tatizo lolote walilolipata kutoka kwenye bidhaa waliyonunua kutoka kwa wauzaji hivyo kuwawezesha Yara kutoa ufumbuzi wa haraka," alisema Maditto.

Aliipongeza Kampuni ya Yara kwa mradi wa kutoa msaada wa mbolea ili kusaidia matatizo ya kiuchumi yaliyosababishwa na janga la Covid-19 kwa mwaka jana ambao ulipewa jia la 'Action Africa' na Mkoa wa Mbeya pekee ulipewa tani 1,683 kati ya 13,951 zilizotolewa msaada nchi nzima.

"Ni matumaini yetu sisi kama serikali wakulima wa Mbeya wataendelea kutumia bidhaa za Yara na kama ilivyoelezwa kupitia programu hii italeta manufaa kwa wauzaji kwa upande mmoja na wakulima upande mwingine, hivyo ni matumaini yetu kuwa wadau wote watatumia 'App' hii vizuri kwa malengo ya kupata ufanisi na maendeleo zaidi katika kilimo chetu hapa Mbeya," alisema.

Meneja usuluhishi wa kidigitali wa Yara, Deodath Mtei, alisema programu hiyo itawasaidia wafanyabiashara hao kuaminika kwa wateja wao kwa kuwa mkulima huwa na desturi ya kuwa na imani na utulivu endapo kwa muuzaji ambako maswali yake yatajibiwa kwa usahihi.

"Ninyi ni mabalozi wetu, mpo karibu zaidi na walengwa wa bidhaa zetu ndio maana kupitia 'App' hii tumeanzisha mpango wa uaminifu wa malipo kwa wafanyabiashara wa rejareja ili kuwapa pointi kwa mauzo myafanyayo kupata zawadi mbalimbali kuanzia simu za mkononi, pikipiki na fedha taslimu," alisema.

Akijibu baadhi ya maswali kuhusu ubora wa mbolea ya Yara, Bwana Shamba Mwandamizi wa Yara, Maulidi Mkima, alisema ili kupata matokeo bora ni vyema wakulima wakaelekezwa kufuata kanuni zote za matumizi ikiwamo vipimo na wakati sahihi wa matumizi ili kuepuka matokea yasiyoridhisha.

Naye mmoja wa wauza mbolea wa Mbeya, Daudi Nyassa, aliiomba serikali kuangalia tatizo la kupanda kwa bei ya mbolea kila mara na pia kushuka kwa bei ya mazao kipindi cha mavuno jambo linaloleta athari kwa wakulima na kwa wauza pembejeo za kilimo.

"Mkulima anaponunua pembejeo kwa bei za juu kisha akauza mazao yake kwa bei ya chini hataweza kurudisha gharama za uzalishaji hivyo kufanya kilimo kisichokuwa na tija jambo ambalo litaweza kuleta athari katika mnyororo wote wa thamani wa kilimo chini," alisema Nyassa.



# Makosa 1,480 barabarani yaripotiwa Juni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKOSA 1,484 ya barabarani yameripotiwa kwa mwezi wa Juni, mwaka huu, huku moja kati ya hayo likiwa limefanywa na dereva mwanamke.

Hayo yalisemwa jana na Asha Mussa Mahfoudh kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Kitengo cha Makosa ya Jinai, Madai na Jinsia wakati akiwasilisha taarifa ya makosa ya barabarani kwa mwezi wa Juni kwa waandishi wa habari.

Alisema Wilaya ya Kati Unguja ina idadi kubwa ya makosa ya barabarani ikiwa na makosa 295 sawa na asilimia 19.9 kati ya yote yaliyoripotiwa.

Kwa mujibu wa Asha, Wilaya ya Kusini Unguja ina idadi ndogo ya makosa ya barabarani yaliyoripotiwa ambayo ni 33 sawa na asilimia 2.2.

Hata hivyo, alisema katika makosa hayo ya barabarani, ajali zilikuwa 14 na kwamba zimepungua ikilinganishwa na Mei, mwaka huu.

Alisema katika ajali hizo zilizoripotiwa Juni, mwaka huu, waathirika walikuw 20 ambapo 14 walikuwa wanaume na sita wanawake.

Pia alisema waathirika wengi zaidi wa ajali hizo waliojeruhiwa na kufariki dunia ni watembea kwa miguu 11, waendesha baiskeli na pikipiki sita na madereva wa magari watatu.

Asha alisema kuwa chanzo cha ajili hizo ni mwendokasi wa madereva ambao baadhi yao wamekuwa wakiendesha vyombo vya moto wakiwa wamelewa.

Naye Koplo Ali Abdallah kutoka Kikosi cha Usalama Barabarani Makao Makuu ya Polisi Zanzibar, aliwapongeza madereva wanawake ambao wamekuwa umakini zaidi kuliko madereva wanaume wanapokuwa barabarani.

"Madereva wanawake wako vizuri katika kutii sheria za barabarani. Tunawaomba madereva wanaume kuiga mfano wa madereva wanawake ili kupunguza ajali na makosa ya barabarani," alisema.

Pia aliwataka watembea kwa miguu barabarani kuwa makini kwa sababu wanapaswa kufuata sheria na kuzijua alama na miongozo ya kutembea hasa wakati wa kuvuka barabara kutoka upande mmoja kwenda mwingine.

## Waziri ataka vikao kutatua kero kazini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, amewaagiza wakurugenzi wa idara za wizara hiyo kufanya vikao vya mara kwa mara na watendaji ili kujua matatizo yanayowakabili.

Aliyasema hayo alipofanya kikao na wafanyakazi wa wizara hiyo huko Mazizini Unguja na kusisitiza kuwa hali hiyo itasaidia kutatua matatizo yao na kuwawezesha kufanya kazi kwa weledi zaidi.

Simai alisema muda umefika sasa kwa kila mtendaji kufanya kazi kwa kufuata sheria za kazi na utumishi serikalini na kuhakikisha kila mmoja atambue wajibu wake.

Alisema wizara imeanza utendaji wake kwa kasi ndani ya mwaka mpya wa bajeti 2021/22, hivyo ni lazima watendaji wote kwenda sambamba na kasi hiyo kwa lengo la kuleta maendeleo ndani ya sekta ya elimu.

Waziri huyo alimwagiza Katibu Mkuu wa Wizara hiyo kuhakikisha usafi wa mazingira unafanyika kila mwisho wa mwezi kama ilivyopangwa awali, huku akimtaka kufanya uhakiki wa wafanyakazi wote wa wizara ili kujua taarifa zao.

Aidha, aliwataka watendaji wa wizara hiyo kuachana na tabia ya kufanya ofisi sehemu ya mazungumzo na kuacha kutumia mitandao kwa mambo yasiyo maana na badala yake kutumia kubuni masuala mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya elimu nchini.

Akizungumzia ugatuzi kurudishwa Wizara ya Elimu alisema ni lazima wizara ijipange kuhakikisha wanapunguza changamoto mbalimbali zilizokuwa zikijitokeza ili kuona maendeleo yanapatikana kwa wote.




Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC), Arafat Haji (kushoto) na Kaimu Posta Masta Mkuu wa Shirika la Posta nchini (TPC), Macrice Mbodo (kulia), wakitia saini hati ya makubaliano ya kiutendaji baina ya mashirika hayo mawili, mjini Zanzibar. Wanaoshuhudia ni Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar, Dk. Juma Malik Akili (kushoto waliosimama nyuma), Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Amour Hamil Bakari (kulia waliosimama nyuma) na Mwenyekiti wa Bodi ya ZIC, Balozi Juma Abdallah Ali (katikati). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bandari kuwekwa mfumo kidijitali

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar, imesema itaweka mfumo mmoja wa taarifa katika Bandari ya Zanzibar ili taasisi zote zilizoko katika taasisi hiyo zifanye kazi vizuri.

Waziri wa Fedha na Mipango wa Zanzibar, Jamal Kassim Ali, aliyasema hayo jana wakati akizungumza katika ziara aliyoifanya katika Bandari ya Malindi, Zanzibar.

Alisema bado kuna tatizo la namna bora ya taarifa zinazotoka mamlaka moja kwenda nyingine kupelekwa kwa mifumo ya karatasi hali ambayo inasababisha usumbufu kwa wafanyabiashara, hivyo kuchelewa kupata mizigo na kusababisha urasimu.

Kutokana na tatizo hilo, Waziri Jamal alisema serikali inataka kuweka mfumo mmoja wa kiteknolojia ambao utasaidia kwa kiasi kikubwa mapato ya serikali kukusanywa kwa ufanisi.

Pia alisema mfumo huo utapunguza gharama na muda unaotumika katika kupeleka taarifa na kuwezesha muda wa kuondoa makontena unakuwa mfupi.

Alisema wiki ijayo wataita wataalamu ambao wako nchini ambao wametengeneza mifumo mingi ikiwamo ZAN Malipo na mifumo ya ZRB ili kutengeneza mfumo huo ambao utakuwa wa kidijitali utakaoleta ufani si katika shirika hilo.

"Lazima hapa tutengeneze mfumo unaokwenda na wakati kuona mambo yote yanafanyika kwenye kompyuta. Hatutaki tena mambo ya makaratasi. Sasa tupo katika dunia ya sayansi na teknolojia, makara tasi yanatuchelewesha," alisema.

Alisema mfumo huo unalenga kuboresha huduma za bandari hasa katika kuwarahisishia wafanyabiashara kupata mizigo yao kwa wakati.

Waziri Jamal alipongeza jitihada zinazochukuliwa na uongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar za kupatia ufumbuzi kero ya mrundikano wa makontena ambalo kwa sasa limepungua kwa kiasi kikubwa na kuwaomba kuendelea kuifanya kazi hiyo kwa ufanisi ili makontena yasichukue muda mrefu kukaa bandarini.

"Tunajua kwamba wana uhaba wa nafasi na vitendea kazi havitoshelezi lakini wajitahidi katika jambo hili la kupakua na kupakia makontena ili kutoa fursa kwa wafanyabiashara kushusha mizigo yao mingi hapa," alisema.

Pia alisema bandari ni sehemu muhimu na lango kuu la uchumi wa nchi hususan kwa Zanzibar ambayo imezungukwa na visiwa.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha Bandari ya Zanzibar inafanya kazi kwa ubora na ufanisi mkubwa ambao utawezesha mizigo mingi kuja Zanzibar na kusafirishwa kupitia hapo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA INAUZWA

IPO KIJITONYAMA ALIMAUA 'A' INA VYUMBA 3 VYA KULALA KIMOJA MASTER,ENEO 700SQM KANDOKANDO YA BARABARA YA LAMI KUNA GEREJI YA GARI NA DUKA,BEI TSH 160M

**SIMU.0782 574669 / 0621 879477**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

**JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA MAGU**
**KITUO CHA MAGU MJINI MKOA WA MWANZA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI NA 24. 2021**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI**
**MAREHEMU....SAMI JOHN BUGARIKA ....WA... MAGU**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA.....ESTHER SAMI JOHN**

**TANGAZO**

(kanuni ya 5(2) ya usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 04 mwezi 08 mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa

Imetolewa leo tarehe 14 mwezi wa 7 mwaka 2021

*116360802*

## KUPOTEA KWA CHETI



**EVANCE LUGALA** anatangaza kupotelewa na cheti cha chuo cha **MEDICAL LABORATORY SCIENCES kozi ya DIPLOMA YA MAABARA** chenye registration namba **NS0147/0121/2009** kilichotolewa na chuo cha **MVUMI/DODOMA** mwaka 2021,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Polisi taarifa LOMB/RB/393/021**

*116360202*

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GODFREY FRENK BOMANI** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye jina **GASTO IGNAS NDUNGULU** namba za usajili **T 344 AGG** aina ya **TOYOTA HIACE** Chassis No. **LH71B0002727**,Engine **No.2L1321843.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi **DOD/RB/3814/19.**

*116361002*

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SAID ISMAIL KILONGO** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **TIANDA** yenye namba za usajili **MC 123AQL.**Chasis **No. LTZPCKLN4E5510014** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/R-B/352527/2021.**

*116360902*

## KUPOTELEWA NA OFA YA KIWANJA

**ZAINA MIKIDADI MWATIMA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA OFA YA KIWANJA CHENYE NAMBA 10/44 ENEO LA MAJENGO,MTAA WA BAHATI.YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/347594/2021.**

*116360702*

AJ RECOVERIES LTD
Your vision our future

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na **LETSHEGO BANK(T)LIMITED–,**tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara nyumba ya mdaiwa wa **LETSHEGO BANK TAWI LA MANZESE,** kama inavyoonekana hapa chini,

| S/NO | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | MAHALI ILIPO | SIKU ,TAREHE,MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | VALENCY CHARLES KALANGA | NYUMBA (Plot no.726,Block "C",Madale,Manispaa ya Kinondoni.) | Mtaa - Madale<br>Kata - Wazo<br>Eneo - Mitikini | Siku -Ijumaa<br>Tarehe -16/07/2021<br>Muda -Kuanzia saa Tano (5) Asubuhi. |

**MASHARTI YA MNADA:**

1. Mnunuzi atalipia sio chini ya asilimia 25% ya bei ambayo imefikiwa siku ya mnada na kiasi kilicho baki anataki wa kumaliza ndani ya siku kuminanne(14),endapo atashindwa kumalizia salio lililobaki mnada utarudiwa upya na fedha iliyolipwa haitarudishwa.Ukaguziwa dhamana ni kwa kuwasiliana na dalali au Tawi la benki Husika siku yoyote muda wa kazi.
2. Gharama za kubadilisha umiliki wa dhamana ni ya Mnunuzi.
3. Dhamana itauzwa jinsi ilivyo.

**MAWASILIANO ZAIDI AJ RECOVERIES LIMITED -0686 153126 / 0788 214 220**

*116360102*

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Wapewa wiki mbili kudhibiti majitaka

**Na Mwandishi Wetu,** MBINGA

NAIBU Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), ameitaka migodi ya uchimbaji wa makaa ya mawe ya Tancoal Ltd na Ruvuma Coal kudhibiti majitaka.

Hamad Hassan Chande amesema uwekezaji wowote ni lazima uzingatie Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 na kanuni zake ikiwa ni pamoja kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa kuwa ni matakwa ya kisheria.

Akiwa ziarani wilayani Mbinga mkoani Ruvuma jana, Chande alitoa siku 14 kwa Mgodi wa Tancoal kudhibiti maji taka katika mabwawa yao pamoja na kudhibiti vumbi ambalo limekuwa kero kwa wakazi wa maeneo ya jirani.

"Mazingira ndiyo uhai wetu, tuyatunze na tuyalinde kwa gharama yoyote ile," Chande aliagiza.

Naibu waziri huyo alishuhudia ukataji wa miti kwa kiwango kikubwa katika migodi hiyo na kuagiza migodi yote miwili kuandaa mpango wa muda mfupi wa upandaji miti ili kurejesha uoto wa asili.

Pia aliagiza migodi hiyo ya makaa ya mawe kuhakikisha inaandaa na kutekeleza mpango madhubuti wa kurejesha ardhi katika hali ya awali baada ya shughuli za uchimbaji kukamilika ikiwa ni pamoja na kupanda miti kwa wingi.

"Upandaji miti uwe ni utamaduni wetu, hapa mgodini miti mingi imekatwa, wekeni mkakati wa kuirejesha kipindi cha mvua," aliagiza.

Katika hatua nyingine, Chande alimwagiza Meneja wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira Kanda ya Kusini, Jamal Baruti, kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kuhakikisha masuala ya uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira yanakuwa endelevu.

Akiwasilisha taarifa ya Wilaya ya Mbinga, Mkuu wa Wilaya hiyo, Aziza Mangosongo, alisema jitihada na mikakati mbalimbali imechukuliwa katika kudhibiti vitendo vya uchafuzi na uharibifu wa mazingira unaosababishwa na shughuli za uchimbaji wa madini.

Shughuli za uchimbaji, uchakataji na uuzaji wa madini ya makaa ya mawe wilayani Mbinga zilianza mwaka 2012 kupitia Kampuni ya TanCoal Energy Ltd na siku za hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la kampuni zinazojikita katika utafiti na uwekezaji kwenye Sekta ya Madini.

# Mhadhiri: Kina Mdee waende mahakamani

**Na Enock Charles**

SIKU moja baada ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kuweka bayana msimamo wake kuhusu wabunge 19 wa viti maalum waliotokana na chama hicho, baadhi ya wadau wa siasa wamewashauri wabunge hao kulipeleka suala hilo mahakamani.

Akizungumza na Nipashe jana, Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. George Kahangwa, alisema mahakama ndicho chombo sahihi cha kukata rufani kwa wabunge hao kama wanaona haki yao imepokwa.

"Sidhani kama sehemu sahihi ya rufani yao ni kwa Msajili wa Vyama vya Siasa, labda ingekuwa mahakamani.

"Watanzania ndiyo wanaogharamia wabunge. Sasa, kama hawana uhalali, maana yake wanakula haramu, tulipaswa kufuata haki badala ya kuingia kwenye ushindani wa kisiasa," alihadharisha.

Dk. Kahangwa pia aliitaka CHADEMA kusikiliza haraka rufani ya wabunge hao kama katiba ya chama hicho inaruhusu ili kuondoa sintofahamu.

Alisema huenda wabunge hao wamechoka kusubiri kuwekwa katika kile alichokiita 'mabano'.

Wakili wa Kujitegemea, Jebra Kambole, akizungumzia suala hilo, alisema kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa ya Mwaka 2019, Msajili ni mlezi wa vyama na wala si msimamizi wa vyama.

Alishauri kuwa kuna haja Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kuhakikisha vyama haviingiliwi katika majukumu yake ya ndani.

"Utaratibu wa nchi upo katika Katiba na Sheria ya Vyama vya Siasa na hata wakienda mahakamani, bado watatakiwa kusubiri kwanza uamuzi wa mwisho kutoka katika chama chao ambao bado haujafanyika," alifafanua Kambole. Juzi, Naibu Katibu Mkuu wa CHADEMA Bara, Benson Kigaila, akizungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam, alisema wamepokea barua ya Msajili wa Vyama vya Siasa ikiwataka kueleza sababu za kuwafukuza ubunge wabunge 19 wa viti maalum wanaotokana na chama hicho.

Kigaila alisema chama hicho kimemjibu Msajili kwamba hakitawasilisha kwake maelezo kuhusu uamuzi huo kwa kuwa katika barua yake, hakuambatanisha vielelezo alivyodai kuvipata kutoka kwa walalamikaji.

Desemba mwaka jana, wanachama 19 wa CHADEMA waliapishwa kuwa wabunge wa viti maalum akiwamo aliyekuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa CHADEMA (BAWACHA), Halima Mdee, Makamu Mwenyekiti wa Baraza hilo, Hawa Bananga na vigogo wengine kutoka baraza hilo licha ya uongozi wa juu wa chama hicho kupinga suala hilo.

Spika wa Bunge, Job Ndugai, alishaweka wazi kwamba hawezi kuwafukuza wabunge hao kwa kile alichodai kutokupata barua ya uthibitisho wa uamuzi wa kufukuzwa uanachama uliofanywa na chama chao.




Mwenyekiti wa Kikundi cha Amani wilayani Kyela, mkoani Mbeya, Shida Ilondo (kushoto), akipokea cheti kutoka kwa Ofisa Kiungo wa Mradi wa Mwanamke Jasiri ambaye ni Ofisa Maendeleo ya Jamii wa wilaya hiyo, Amos Kayembela, wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wanawake kutambua haki zao, jana **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# NHC yatakiwa kubuni miradi mipya

**Na Munir Shemweta,** MOROGORO

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC) mkoa wa Morogoro limetakiwa kubuni miradi mipya ya ujenzi ili kuliwezesha kuingiza fedha badala ya kutegemea nyumba zilizopo ambazo ni za kizamani.


Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, alitoa agizo hilo juzi mkoani hapa wakati akizingumza na watumishi wa shirika hilo mkoani hapa wakati wa ziara ya kusikiliza na kuzitafutia ufumbuzi kero za ardhi.

Alisema haileti maana NHC kutegemea nyumba zilizojengwa na mkoloni bila kuwa na mipango mipya ya ujenzi itakayowezesha shirika kuwa na nyumba za kisasa zitakazoiwezesha kujiongezea kipato.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, mkoa wa Morogoro bado una uhitaji mkubwa wa nyumba zikiwamo zile za kupangisha hasa kwenye maeneo mapya na kusisitiza kuwa NHC haina budi kuongeza kasi kwa kubuni miradi mipya kwa ajili ya kutosheleza mahitaji hayo.

"Kumbe ninyi bado mko kizamani, yaani hamna mradi wa ujenzi wa nyumba mpya na mnategemea zile za zamani? Mnatakiwa kujiongeza kwa kubuni miradi mipya ili kuongeza mapato ya shirika," alisema.

Naibu Waziri alimtaka Meneja wa NHC Morogoro, Constantine Yuda, kwenda katika halmashauri za mkoa huo ili kupatiwa maeneo kwa ajili ya ujenzi wa miradi mipya ikiwamo ya nyumba za watumishi kwenye halmashauri za mkoa huo.




# CHIELLINI BADO AISIKILIZIA JUVENTUS

**TURIN,** Italia

WAKALA wa Giorgio Chiellini amesema wanaisubiria Juventus kujadiliana kuhusu mkataba mpya, huku akisema suala la kustaafu soka kwa nahodha huto wa Italia aliyeshinda Euro 2020 ni "ukichaa".

Chiellini, ambaye atatimiza umri wa miaka 37 mwezi ujao, ni mchezaji huru kwa sasa baada ya mkataba wake na Juventus kumalizika mwanzoni mwa mwezi huu.

Mlinzi huyo mkongwe alikuwa mhimili mkubwa wa kikosi cha Italia katika mbio za kushinda Euro 2020.

Iliripotiwa kwamba, Chiellini atasaini mkataba mpya na kibibi kizee hicho cha Turin kwa ajili ya msimu 2021-22 ingawa wakala wake, Davide Lippi amebainisha kwamba mazungumzo hayajaanza na wanasikiliza ofa kutoka klabu nyingine.

"Hakuna kilichofanyika kwa sasa," alisema wakala Davide Lippi akiiambia Radio Radio.

"Giorgio alikwenda kwenye Euro na alijizatiti kule. Hakuna tatizo na Juventus, tulisema tutakutana baadaye wakati wa kipindi cha majira ya joto, lakini hatujakaa chini na kujadiliana kuhusu mkataba mpya."

Katika ofa kutoka katika klabu nyingine, Lippi aliongeza: "Zinatakiwa kwanza kutoa ofa. Kama nilivyosema, hakuna mtu. Tunasubiri Juventus kutuambia lini tutakaa nao chini na kuzungumza."

Lippi pia alisema ni uchizi watu kuzungumzia kustaafu soka kwa Chiellini baada ya kutwaa taji la Ulaya.

# DONNARUMMA asajiliwa rasmi PSG

**PARIS,** Ufaransa

PARIS St-Germain imekamilisha usajili wa golikipa wa Italia, Gianluigi Donnarumma kwa uhamisho huru.

Kipa huyo mwenye umri wa miaka 22 anajiunga na PSG baada ya kutoka kutajwa mchezaji bora wa mashindano wakati Italia ikishinda taji la Euro 2020, Jumapili iliyopita.

Aliokoa penalti mbili wakati Azzurri ikiifunga England kwenye changamoto ya mikwaju hiyo.

Donnarumma, ambaye amesaini mkataba wa miaka mitano hapo PSG, alitangaza mapema wiki hii kwamba, anaondoka AC Milan baada ya mkataba wake kumalizika.

"Nina furaha kubwa kuwa sehemu ya klabu kubwa," alisema.

"Najihisi kuwa tayari kuchukua changamoto hii mpya, na kuendelea kukua hapa.

"Nikiwa na Paris, nataka kushinda kadili inavyowezekana na kuwapa furaha mashabiki."

Donnarumma amecheza mechi 33 kwa Italia na amekuwa golikipa chaguo la kwanza chini ya kocha, Roberto Mancini.

Amecheza mechi 251 kwa Milan katika mashindano yote tangu alipoanza kuichezea mara ya kwanza akiwa na umri wa miaka 16.

Alicheza mechi zote kasoro moja kwenye Ligi Kuu ya Italia msimu wa 2020-21, akiwasaidia Milan kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza baada ya miaka saba.



# Real Madrid yapata hasara pauni mil. 256



**MADRID,** Hispania

REAL Madrid imebainisha kupoteza "karibia pauni milioni 256" kwenye mapato wakati wa mlipuko wa virusi vya corona wakati matokeo yao ya kifedha yaliyotangazwa jana.

Lakini Los Blancos hao wameripotiwa kupata faida ya kodi ya pauni 746,000 kwa msimu wa 2020-21, kutoka 267,000 waliyoipata mwaka wa fedha uliopita.

Mabingwa hao mara 13 wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hawakufanya usajili wowote msimu wa 2020-21 huku wakimuuza Achraf Hakimi na Sergio Reguilon na kumruhusu James Rodriguez kuondoka.

Majina mengine makubwa yamefuata mwaka huu, huku Sergio Ramos akiondoka baada ya kunyimwa mkataba wa muda mrefu na Raphael Varane anaweza kuondoka, kwani anahusishwa sana na Manchester United.

Hata hivyo, Madrid hawafikirii kuingi kwenye hali ya kimtego kama kwa wapinzani wao Barcelona, ambao wanakaribia kufikia kumpa mkataba mpya Lionel Messi lakini lazima wasafishe kwanza chumba chao kutokana na tatizo la mishahara mikubwa.

Na Los Blancos – ambao uwanja wao wa Santiago Bernabeu upo kwenye ukarabati na timu ilikuwa ikicheza sehemu nyingine wakati huu wa mlipuko wa virusi vya corona pia inamwania Kylian Mbappe.

Taarifa ya klabu hiyo kwa waandishi wa habari ilisomeka: "Kutokana na hali ya kiuchumi, hali ya sasa inaashilia kwamba, hali haitaimarika haraka kutokana na mlipuko wa virusi vya corona."

## HABARI MICHEZO



# Maldini: Giroud anakaribia kutua Milan

**MILAN,** Italia

MKURUGENZI wa AC Milan, Paolo Maldini amethibitisha Olivier Giroud anakaribia kujiunga na miamba hao wa Serie A akitokea Chelsea.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 34 ametumia miaka mitatu na nusu akicheza pale Stamford Bridge na hivi karibuni aliongezewa miezi 12 kwenye mkataba mpya ili kuendelea kubakia kwa Blues hao.

Giroud alianza katika mechi 12 tu kwenye mashindano yote msimu uliopita, lakini alimaliza kama mfungaji bora wa Chelsea wakati wakishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na mabao sita, na Timo Werner na Tammy Abraham pekee ndio walifunga mabao mengi zaidi kwenye mashindano yote (wote 12).

Milan imeripotiwa kukubali ada ya euro milioni 3 kumsajili kutoka Chelsea, huku wakimpa ofa ya miaka miwili Giroud.

"Olivier anaweza kuwasili kesho (jana)," alisema Maldini akiiambia DAZN jana.

"Olivier ni bingwa. Amefanya mambo makubwa akiwa na Ufaransa na Chelsea.

"Ni mchezaji mkubwa na mwenye kipaji na tunaangalia namna atakavyoweza kukisaidia kikosi chetu kilichojaa wachezaji vijana."

Mchezaji huyo anatarajia kuongoza safu ya ushambuliaji ya kocha Stefano Pioli wakati Zlatan Ibrahimovic akiwa anajiuguza majeruhi ya goti na kumfanya akose kuichezea Sweden kwenye Euro 2020.

# Sancho avunja ukimya



**LONDON,** Engand

JADON Sancho amevunja ukimya baada ya kukosa penalti kwenye fainali ya Euro 2020 na kujikuta akiandamwa na ubaguzi wa rangi kwenye mitandao ya kijamii.

Winga huyo wa England aliingizwa katika dakika za mwisho za muda wa nyongeza dhidi ya Italia wakati mchezo huo ukisomeka 1-1.

Sancho na Marcus Rashford walionekana waliingizwa kwa ajili ya mikwaju ya penalti na wote walikuwa kwenye orodha ya wachezaji wa kupiga penalti tano za kwanza.

Lakini baada ya Rashford penalti yake kugonga mwamba, ile ya Sancho iliokolewa na golikipa Gianluigi Donnarumma.

Kabla ya penalti ya Bukayo Saka nayo kuolewa na kuifanya Italia kushinda taji hilo kwa penalti 3-2.

Sancho na wachezaji wenzake ambao wote ni weusi walikumbwa na kashfa nyingi kwenye mitandao ya kijamii hadi chama cha soka cha England kuingilia kati.

Sancho akizungumza kwa mara ya kwanza kuhusiana na kashfa hizo baada ya kukosa penalti, Sancho ambaye amekamilisha usajili wa kutua Manchester United kutoka Borussia Dortmund, alisema alijiamini.

"Nilikuwa na siku kadhaa za kufikiria kile kilichotokea kwenye fainali na bado nina mkanganyiko wa hisia," aliandika Sancho kupitia ukurasa wake wa Instagram.

# Griezmann kubadilishwa na Niguez

**MADRID,** Hispania

NYOTA wa Barcelona, Antoine Griezmann anatarajia kurudi Atletico Madrid kipindi hiki cha majira ya joto baada ya klabu hizo mbili kufikia makubaliano ambayo yatamfanya Saul Niguez kutua Camp Nou.


La Blaugrana wapo kwenye mpango wa kupunguza bili ya mishahara mikubwa kwa wachezaji wake na kwa sasa nyota huyo wa Ufaransa ndiye analipwa mshahara mkubwa zaidi, huku Lionel Messi akiwa bado hajasaini mkataba mpya na miamba hao wa Katalunya.

Barça hawatakuwa tayari kuingia nao makubaliano wachezaji wao wapya wanne au kumpa mkataba mpya Messi hadi wapunguze bili yao ya mishahara ya euro milioni 200 kwa mwaka na hivyo wanataka kuwaondoa wachezaji wengine.

Na sasa wanakaribia kumuuza Griezmann, ambaye anaingiza kiasi cha euro milioni 25 kwa msimu, kwa Atletico ambako aliondoka kule mwaka 2019.

Diego Simeone na benchi lake la ufundi wamesaini mkataba mpya na Atletico Madrid ambao utawaweka hapo hadi mwaka 2024.

Kwa mujibu wa El Partidazo de COPE, makubaliano kati ya klabu hizo mbili yamefikia na itashuhudia Griezmann akirudi Madrid na kiungo Saul akielekea Katalunya.



## KWA UFUPI

### TRIPPIER KURUDI EPL

MLINZI wa pembeni wa England na Atletico Madrid, Kieran Trippier anatarajia kurejea kwenye Ligi Kuu ya England, EPL, huku nyota huyo mwenye umri wa miaka 30 akitajwa kuelekea Manchester United. (**Telegraph**)

### KOULIBALY KULEKEA EVERTON

EVERTON imewasilisha dau la mwanzo la kumsajili mchezaji wa Napoli na Senegal, Kalidou Koulibaly mwenye umri wa miaka 30 ambaye anaripotiwa kuwa miongoni mwa wachezaji wanaolengwa na kocha, Rafa Benitez.(**Calciomercato**)

### BARELLA AWANIWA LIVERPOOL

LIVERPOOL inatarajia kutenga pauni milioni 60 kwa ajili ya kiungo wa kati wa Inter Milan, Nicolo Barella mwenye umri wa miaka 24. (**La Repubblica**)

### ABRAHAM CHAMBO KWA HAALAND

CHELSEA inataka kumtoa ofa mshambuliaji, Tammy Abraham mwenye umri wa miaka 23, kwenda Borussia Dortmund kama sehemu ya makubaliano ya kumchukua mshambuliaji, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 20. (**Mirror**)

### AREOLA KUTUA WEST HAM

KLABU ya West Ham inakaribia kufikia makubaliano ya kumchukua kwa mkopo golikipa wa Paris St-Germain, Alphonse Areola mwenye umri wa miaka 28, huku kukiwa na kipengele cha kumsajili moja kwa moja baadaye. (**Evening Standard**)

### BELLERIN HUYO INTER

MLINZI wa Arsenal, Hector Bellerin bado hajakubaliana na Inter Milan, lakini klabu hiyo ya Italia ina mpango wa kumnasa nyota huyo wa Hispania mwenye umri wa miaka miaka 26. (**Football.london**)

### WILLOCK KURUDI NEWCASTLE

KIUNGO wa kati wa Arsenal, Joe Willock mwenye umri wa miaka 21, ameripotiwa kuiambia klabu hiyo kwamba atajiunga tena na Newcastle kwa mkopo kwa ajili ya msimu mpya wa ligi Kuu ya England. (**Daily Express**)

### TIELEMANS KUPEWA MKATABA

LEICESTER City wametoa ofa kwa mchezaji wa Ubelgiji, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 24 ya mkataba wa muda mrefu na wanaamini kiungo huyo wa kati atasalia katika klabu hiyo, ingawa Liverpool wanamuhitaji pia.(**Telegraph**)

### GRIEZMANN NA NIGUEZ


BARCELONA wanakaribia kukamilisha mpango wa kumpeleka mshambuliaji wa Ufaransa, Antoine Griezmann mwenye umri wa miaka 30, Atletico Madrid ili iweze kumnasa kiungo wa kati wa klabu hiyo, Saul Niguez mwenye umri wa miaka 26. (**Mail**)

### SPURS YAMTAKA HOPPE

TOTTENHAM Hotspur ni miongoni mwa klabu nne za Ligi Kuu ya England zinazomwania mshambuliaji wa Schalke, Matthew Hoppe mwenye umri wa miaka 20, aliyefunga mabao sita na klabu hiyo ya Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, msimu uliopita. (**The Boot Room**)

### MALEN AOTA MBAWA ARSENAL

ARSENAL inajiandaa kumkosa mshambuliaji wa PSV Eindhoven, Donyell Malen mwenye umri wa miaka 22 raia wa Uholanzi, baada ya kufikia makubaliano ya kujiunga na Borussia Dortmund kama mbadala wa Jadon Sancho. (**Just Arsenal via Sports Bild**)



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI AKUBALI KUBAKI BARCELONA HADI 2026

**BARCELONA,** Hispania

### ●●● Nyota wengine kuuzwa ili kugharamia mshahara wake hata...

LIONEL Messi amekubali kusalia Barcelona katika mkataba mpya ambao utamfanya kukaa hapo hadi mwaka 2026, huku pia akipunguziwa mshahara wake, kwa mujibu wa ripoti ya vyombo vya habari vya Ulaya.

Tangazo hilo linategemea kuondoka kwa wachezaji wengine ambapo itaiwezesha Barca kufadhili mshahara wa nahodha huyo wa Argentina.

Messi mwenye umri wa miaka 34, alikuwa mchezaji huru baada ya mkataba wake aliokuwa akilipwa pauni milioni 123 kwa msimu kukamilika Juni 30, mwaka huu.

Kwa sasa mchezaji huyo yupo likizo baada ya kushinda kombe la Copa America na maelezo ya ndani kuhusu mkataba huo mpya bado hayajawekwa hadharani.

Kumshawishi Messi kusalia katika klabu hiyo ndio lililokuwa lengo la rais mpya wa Klabu hiyo, Joan Laporta.

Barca pia inatazamia makubaliano ya kubadilishana wachezaji yanayohusisha uhamisho wa mshambuliaji Antoine Griezmann na kiungo wa kati wa Atletico Madrid, Saul Niguez, ili kupunguza bili ya mishahara ya wachezaji.

**Wchezaji kama vile Junior Firpo, Jean Clair Todipo na Carles Alena tayari wameuzwa ili kupunguza matumizi, lakini uuzaji wa wachezaji wenye majina makubwa pia utafanyika.**

Messi alihusishwa na uhamisho wa kuelekea PSG na Manchester City, ambapo angekutana tena na kocha wake wa zamani pale Barcelona, Pep Guardiola , pamoja na Ligi Kuu ya Marekani, MLS, ambapo alisema kwamba huenda akaichezea katika siku za usoni.

Messi ndiye mfungaji bora wa muda wote Barcelona akiwa na magoli mabao 672 na kushinda mataji 10 ya La-Liga, mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, mataji saba ya Copa del Rey pamoja na kutwaa tuzo ya Ballon d'Or mara ya sita.

HABARI MICHEZO

# MWANARIADHA AKHWARII AHOFIA KUFA BILA KULIPWA

**Na Abdallah Khamis,** MANYARA

MWANARIADHA mkongwe nchini, John Stephen Akhwarii, amesema anahofia kufa akiwa bado hajapatiwa haki yake ya dola 1,000, zilizochukuliwa na serikali mwaka 1963, baada ya kurejea nchini akiwa mshindi wa pili wa mashindano ya riadha ya kimataifa yaliyofanyika Athens nchini Ugiriki.

Akizungumza katika mahojiano maalum na mwandishi wa habari hii nyumbani kwake katika kitongoji cha Khaday, Wilaya ya Mbulu, Mkoa wa Manyara, Akhwari, amesema ameshafanya jitihada za kumfikishia Rais malalamiko yake bila kupata majibu.

Akhwarii alisemwa mwaka 1963, alirejea nchini akiwa mshindi wa pili katika mashindano ya kimataifa ya marathon na kupokewa na waziri wa michezo wa wakati huo, Lawi Nangwanda Sijaona, aliyeambatana na katibu wa chama cha Riadha wakati huo, Khalifa Abdallah pamoja na waandishi wa habari.

Alisema baada ya waziri kufika uwanjani na ugeni wake, alimtaka kupiga nae picha akiwa ameshika cheki ya zawadi na baada ya tendo hilo la picha waziri akaondoka na cheki.

"Baada ya picha waziri aliivuta ile cheki nilipomuuliza sababu ya kuichukua akaniambia niende ofisini kwake siku inayofuata na nilipoenda nikaambiwa kuwa sheria hainiruhusu kuwa na fedha kiasi kile.

"Lakini zawadi ni haki yangu ile na wakati ule ningeweza kununua hata mabasi makubwa mawili kwa hela ile," alisema Akhwari mwenye umri wa miaka 83 sasa.

Gazeti hili lilipomuuliza Kaimu Katibu Mkuu wa Baraza la Michezo la Taifa, (BMT), Neema Msitha, juu ya hatua walizochukua kuhakikisha Akhwarii anapata stahiki yake, alisema jambo hilo wanalifahamu na kwa sasa linashughulikiwa kiwizara.

Naye Mkurugenzi wa Maendeleo ya Michezo, kutoka Wizara ya Habari Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Yusuf Singo, alisema serikali kupitia wizara ilikusudia kumfanyia jambo kwa ajili ya kumfidia.

Hata hivyo, Dk. Singo alipoulizwa kama watamfidia kiasi hicho katika thamani ya wakati huo, alieleza kuwa ni mapema kujua namna fidia hiyo itakavyokuwa.



Mwanariadha John Stephen Akhwarii akifanya mahojiano na mwandishi wa gazeti hili.

# Chama cha wenye ulemavu kuwa Shirikisho

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

CHAMA cha soka kwa watu wenye ulemavu wa viungo Zanzibar kipo katika mchakato wa mabadiliko ya katiba ili kuwa shirikisho.

Akizungumza na gazeti hili rais wa chama hicho, Hassan Silima, alisema rasimu ya katiba ya sasa tayari ishatua katika ofisi ya mrajisi wa vyama vya michezo Zanzibar kwa ajili ya hatua mbalimbali.

Alisema licha ya mabadiliko ya kutoka chama kwenda shirikisho, lakini kutakuwa na mabadiliko ya muundo wa shirikisho hilo ikiwamo kuwa na wanachama ambao ni klabu za soka.

Alisema kuwa hapo awali chama hicho kilikuwa kikiwajumuisha watu wenye ulemavu mbalimbali lakini hivi sasa kitawajumuisha walemavu wenye mguu mmoja na mkono tu.

"Kwa mujibu wa katiba yetu mpya ambayo tutatambulika kama shirikisho yapo mabadiliko kadhaa ambayo yamefanyika, ikiwamo kuwa na wanachama ambapo kwa hatua ya awali tumeanza na klabu," alisema.

Aidha alisema kuwa jitihada mbalimbali wamezichukua katika kuhamasicha watu wenye ulemavu wa mguu na mkono mmoja kuanzisha klabu za soka ili na wao waweze kutimiza ndoto zao katika michezo kama ilivyo kwa watu wengine.

## Mbio za magari Afrika kufanyika jijini Dar

**Na Saada Akida**

CHAMA cha Mbio za Magari Tanzania (AAT), kimeandaa mashindano ya kimataifa ya Afrika, huku timu 34 zikishiriki mashindano hayo yanayotarajia kuanza rasmi Julai 24, mwaka huu kuanzia Dar es Salaam kuelekea Ubena, Pwani.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mkurugenzi wa Mashindano hayo, Satinder Birdi alisema mwaka huu wamejipanga vizuri na wamejitahidi baada ya kupata washiriki 34, mataifa mbalimbali huku Tanzania wakitia fola kwa madereva 19 kujitokeza.

Alisema ratiba yao itaanza Jumatano ya Julia 21, kwa madereva kwenda kujisajili na Alhamisi ya Julai 22, madereva wataenda kukagua magazine pamoja na barabara ya Ubena.

"Tutaanza sherehe za mashindano hayo Ijumaa Julai 23, kuanzia Dar es Salaam hadi Ubena na Jumamosi ndio tutaanza mashindano yetu rasmi asubuhi kule Ubena," alisema.

"Kabla ya kuanza mashindano hayo asubuhi kutakuwa na vipimo vya dereva ili kupata ni nani anatakiwa kuwa wa namba moja, pia mbio zitakuwa kilometa 220, siku ya kwanza watakimbia 88 na kumalizia 130," alisema Birdi.

Naye Rais wa AAT, Nizar Jivan alisema mwaka huu mashindano hayo yamekuwa ya kipekee baada ya kujitokeza kwa wingi washiriki (madereva) kutoka mataifa mbalimbali.

## Matola: Chikwende bado yupo sana

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA msaidizi wa Simba, Selemani Matola amesema kuwa mchezaji, Perfect Chikwende ni mali ya Simba na bado yupo kwenye kikosi hicho wakiwa na malengo naye ya baadaye.

Kocha huyo alizungumza hayo, kufutia tetesi kuwa mchezaji huyo ameondolewa kwenye kikosi na klabu ya Simba ina mpango wa kusajili mchezaji mwingine badala yake.


Matola amesema Chikwende ni mchezaji mwenye kipaji kikubwa, lakini bado anatatizwa na mazingira, hivyo hawana haraka naye, wanachofahamu baadaye atakuwa vizuri.

"Ni kweli tulifanya mabadiliko, tunamtoa Francis Kahata na kumsajili Chikwende. Hajakuwa vizuri mpaka sasa kwa sababu mazingira bado yanamtatiza, kilichopo tumpe muda azoee kwa sababu ni mchezaji mwenye kipaji kikubwa, atakapozoea atakuwa vizuri sana," alisema Matola.

Chikwenda raia wa Zimbabwe amekuwa hapati nafasi ya kucheza kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara, licha ya kwanza alisajiliwa kwa sababu hiyo.

Mchezaji huyo mwenye uwezo wa kucheza kama mshambuliaji na pia winga zote mbili, alisajiliwa na Simba mwanzoni mwa mwaka huu, baada ya kuonekana kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika akiwa na klabu yake ya zamani, FC Platinum ya Zimbabwe.

# Michezo




Ijumaa Julai 16, 2021
Nipashe

## Messi akubali kubaki Barcelona hadi 2026

HABARI UK. 22




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akipokea jezi ya Timu ya Taifa ya Morocco kutoka kwa Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu la Morocco, Faouzi Lakjaa, alipotembelea eneo la Mchezo wa Mpira wa Miguu la Mohammed wa VI (Mohammed VI Football Complex) kuona uwekezaji wa miundombinu ya mpira uliofanywa katika eneo hilo nchini Morocco Jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# NIYONZIMA AAGWA KWA USHINDI

## Biashara United yajihakikishia nafasi ya pili kufuzu kimataifa...

**Na Adam Fungamwango**

MABAO mawili ya kiungo Feisal Salum, jana yaliiwezesha Yanga kumuaga mchezaji wao Haruna Niyonzima kwa ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Ihefu FC kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Wakati Yanga ikishinda mabao hayo na kujihakikisha nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, timu ya Biashara United kujihakikishia kucheza mechi za kimataifa msimu ujao baada ya kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Prisons kwenye Uwanja wa Nelson Mandela, mjini Sumbawanga.

Feisal alifunga mabao hayo dakika ya 17 na 36 na kuifanya Yanga kufikisha pointi 73 ambazo hazitofikiwa na Azam FC.

Niyonzima aliingia uwanjani katikati ya kipindi cha pili na kupewa kitambaa cha unahodha na kucheza hadi mwisho wa mchezo.

**Akizungumza baada ya kumalizika kwa mechi hiyo, Niyonzima alisema kuwa anawashukuru wa nachama, viongozi na mashabiki wa Yanga, huku akisema anaweza kurejea tena Tanzania kama mchezaji kwa sababu bado ana uwezo wa kucheza soka.**

"Tanzania ni nyumbani, naweza kurudi tena, lakini kwangu mimi nimeifanya Yanga kuwa na mashabiki wengi nchini Rwanda," alisema.

Mabao ya Christian Zigah wa Biashara United na Mohamed Mkopi wa Prisons, yalizifanya timu hizo kutoka sare ya bao 1-1.

Ni matokeo ambayo yanaipa tiketi Biashara United kucheza michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika msimu ujao kwa mara ya kwanza tangu kuanzishwa kwake.

Biashara imefikisha pointi 50 ambazo zimeihakikisha timu hiyo kumaliza nafasi ya nne kwani hazwezi kufikiwa na timu yoyote ile iliyo chini yake.

Coastal Union imepanda hadi nafasi ya 14 kwenye msimamo wa ligi baada ya kuinyuka Mwadui mabao 5-0 kwenye Uwanja wa Mkwakwani, Tanga ikifikisha pointi 37, huku Mtibwa Sugar ikishindwa kuchukua pointi zote tatu, baada ya kulazimishwa suluhu bila kufungana dhidi ya Dodoma Jiji, ikiwa ugenini.

Mbeya City, ikiwa nyumbani, Sokoine, ilipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Gwambina, ikipanda hadi nafasi ya 12 kwa pointi 37 na kuididimiza Gwambina hadi nafasi ya 17.

Polisi Tanzania, ikiwa nyumbani, ilikubali kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar, ukiwafanya wageni hao wapae hadi nafasi ya 11 kwa pointi zao 40.

KMC, ikiwa Uwanja wa Uhuru, iliididimiza shimoni JKT Tanzania kwa kuichapa mabao 5-2, ikiiacha kwenye nafasi ya 15 ambapo inasubiri majaliwa yake kwenye mechi za mwisho, huku Ruvu Shooting ikiiadhibu Namungo FC mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani.

## Hatima Uchaguzi Mkuu wa TFF kujulikana leo

**Na Kulwa Mzee**

MASHABIKI na wapenzi wa soka nchini leo watatega masikio Mahakama Kuu kusikiliza uamuzi wa kusimamisha ama kutosimamisha mchakato wa uchaguzi wa Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF).

Uamuzi huo unatarajiwa kutolewa leo saa nane mchana mbele ya Jaji Edwin Kakolaki baada ya kusikiliza hoja mbalimbali za kubishania kusimamishwa kwa muda uchaguzi huo hadi kesi ya msingi namba 98 itakaposikilizwa.

Mlalamikaji katika shauri hilo ni Ally Salehe na mlalamikiwa ni Bodi ya Wadhamini ya TFF, TFF na Mwenyekiti Kamati ya Uchaguzi ambao wanaomba maombi yatupwe na uchaguzi uendelee.

Aliwasilisha hoja wakili wa mlalamikaji Emiah Mtobesya alidai mteja wake aliondolewa katika mchakato kwenye hatua ya mahojiano, wakati alitakiwa kuhojiwa kisha taarifa zake kuwekwa katika ubao wa matangazo endapo kuna anayepinga awasilishe hoja zake.

Wakili Mtobesya anadai utaratibu umekiukwa na madhara yake hayawezi kufidiwa, mlalamikaji atapata hasara hivyo anaiomba mahakama kuzuia mchakato wa uchaguzi.

Akijibu wakili wa walalamikiwa, Alex Muchunguzi alidai kwamba katika kiapo cha mlalamikaji hakuna hoja za msingi za kuifanya Mahakama ifikie uamuzi wa kutoa zuio la muda la uchaguzi hadi kesi ya msingi namba 98 itakaposikilizwa.

Alidai kutolewa kwa zuio kutamwathiri zaidi mlalamikiwa namba mbili TFF, inaweza kufungiwa na FIFA kushiriki katika mashindano ya mpira wa miguu.

Miongoni mwa masuala anayolalamikia mlalamikaji Ally ni pamoja na upungufu uliyomo katika Katiba ya TFF ikiwamo suala la ubaguzi katika katiba hiyo kuhusiana na zoezi la uchaguzi.

Uchaguzi huo unaotarajiwa kufanyika Agosti 7, mwaka huu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >